Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tatu - Tarehe 10 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):**

Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2003 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2004/2005.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):**

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa mwaka 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 20

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kwangwa**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye miaka ya sabini wananchi wa Mkoa wa Mara waliamua kujitolea kutoa michango ya hali na mali kujenga Hospitali ya Rufaa Kwangwa - Mjini Musoma; na kwa kuwa ujenzi wa hospitali hiyo umesimama kwa muda mrefu; na kwa kuwa michango ya wananchi imekamilisha *structural* ya ghorofa saba; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichangia kukamilisha majengo mbalimbali yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kama madarasa, mpango ambao umefanikiwa kwa kiasi kikubwa:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu kuchangia ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali hiyo ili nguvu za wananchi zisipotee bure?

(b) Je, Serikali iko tayari kupokea maombi na kilio cha wananchi wa Musoma na Mkoa wa Mara kwa ujumla kwamba Serikali itenge fedha za kukamilisha ujenzi huo katika kipindi cha fedha cha 2004/2005?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika miaka ya sabini, wananchi wa Mkoa wa Mara waliamua kujenga Hospitali ya Kwangwa kwa madhumuni ya kuwa na hospitali mpya ya Mkoa ya kisasa na yenye uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi zaidi na sio kuwa Hospitali ya Rufaa. Suala la ujenzi wa Hospitali za Rufaa hushughulikiwa na Wizara ya Afya na kwa upande wa Mikoa ya Ziwa, tayari kuna Hospitali ya Rufaa ya Bugando, ambayo inawahudumia wananchi wa Mikoa hiyo. ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa ulianza rasmi mwaka 1980 na ulikuwa ufanyike katika awamu tatu. Awamu ya kwanza, ilihusu ujenzi hadi kufikia ghorofa ya kwanza na kufanya *partitions* za kugawa wodi za wagonjwa na kujenga nyumba tano za daraja la "A" kwa ajili ya Madaktari na nyumba tano za daraja "B". Awamu ya pili, ilihusu ujenzi wa nyumba 40 za Watumishi na Awamu ya tatu, ilihusu kukamilisha shughuli za nje kama vile ujenzi wa mifereji ya maji machafu. Awamu ya kwanza, ilitarajiwa kugharimu dola za Marekani 2,427,490 kwa gharama za mwaka 1995. Aidha, hospitali ilitarajiwa kuwa na *Blocks 3* za majengo zenye uwezo wa vitanda 500 baada ya kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa ulisimama mwaka 1987 baada ya wananchi kuacha kuendelea kuchangia. Hadi wakati huo, wananchi walikuwa wamechangia shilingi 42,000,000 na Serikali ilitoa shilingi 39,500,000. Mradi huo ulikabidhiwa rasmi Serikalini mwaka 1995 kufuatia maamuzi ya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa, iliyokaa tarehe 17 Septemba, 1993. Hadi sasa ujenzi umefikia ghorofa ya kwanza na Serikali bado inayo nia ya kukamilisha ujenzi wa ghorofa ya kwanza ili iweze kuanza kutumika.

Aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya fedha za kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo, ikilinganishwa na bajeti finyu inayotengwa kwa ajili ya Mkoa, Serikali iliamua kuendelea kuimarisha majengo ya hospitali iliyopo ambayo ni machakavu ili wananchi waendelee kupata huduma. Hata hivyo, Serikali imeendelea kufanya mazungumzo na Wahisani mbalimbali ili kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa. Mazungumzo yalifanyika na Serikali ya Hispania mwaka 1999 na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la *JICA,* pamoja na juhudi zote hizo bado Serikali haijafanikiwa kupata msaada wowote.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ipo pamoja na wananchi wa Mara katika juhudi za kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Kwangwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, je, ni sifa zipi ambazo zinaiwezesha hospitali iweze kufikia kiwango cha kuwa Hospitali ya Rufaa?

La pili, kwa sababu Serikali inaendelea kupeleka fedha kwenye Hospitali ya Mkoa iliyopo ambapo hospitali hii ilijengwa mwaka 1932. Serikali haioni kwamba kuna sababu za msingi fedha hizo sasa kuelekezwa kwenye Hospitali hii ya Kwangwa badala ya kuendeleza majengo yale ambayo kwa kweli ni machakavu na hayastahili tena kuendelea kutumika katika Hospitali ya Mkoa iliyopo sasa hivi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuwa sifa za Hospitali za Rufaa ziko chini ya Wizara nyingine, pengine nitamwomba Naibu Waziri wa Afya ajibu sehemu hiyo ya swali lako. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA) :** Mheshimiwa Spika, utaratibu tuliojiwekea ni kwamba, kwanza tuwe tuna Hospitali za Rufaa Kikanda kabla ya kuendelea katika Mikoa. Kwa hiyo, hivi sasa kanda zote zina Hospitali za Rufaa isipokuwa Kanda ya Kusini na Kanda ya Kati. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kwanza tunapata Hospitali za Rufaa katika Kanda hizo mbili kabla ya kuendelea. Kwa hiyo, kwa Musoma hatuwezi kuwa na Hospitali ya Rufaa kwa hivi sasa. Sifa za Hospitali ya Rufaa ni nyingi, ningependa nimpatie Mheshimiwa Mbunge kwa maandishi. Lakini kwa uchache tu niseme kwamba, idadi ya vitanda, uwezo wa maabara, idadi ya madaktari mabingwa na vigezo vingine kadhaa, vinahusika katika jambo hilo.

**SPIKA:** Bado swali linaendelea kujibiwa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, jibu sehemu ya pili ya swali lake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Hospitali ya Mkoa wa Mara ya sasa ilijengwa mwaka 1932, kwa hiyo ni kweli hospitali hiyo ni ya zamani. Vilevile ni kweli kwamba, hospitali tunayotaka kuijenga inahitaji fedha nyingi ambazo kwa sasa hivi kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, kutokana na ufinyu wa Bajeti, hatuwezi kuikamilisha sasa. Lakini vilevile ni kweli kwamba, katika kipindi hiki hatuwezi kuwaambia wananchi waache kuugua, ni lazima tuendelee kutoa matibabu

mahali. Kwa hiyo ni lazima tuendelee kuihudumia hospitali hii ya zamani na tuendelee kuboresha hali yake mpaka hapo hospitali mpya hii tunayoijenga itakapokamilika.

Na. 21

**Nafasi ya Mgombea Mwenza katika Nafasi za Urais**

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL (k.n.y. MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuwepo kwa Mgombea Mwenza kwenye nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumemwondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na kwa wakati huo kulikuwa na Waziri katika Ofisi ya Rais aliyekuwa akiingia kwenye Baraza la Wawakilishi na Bunge kuhusu masuala ya Muungano: Je, hivi sasa Zanzibar inawakilishwa na nani katika masuala ya Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Dhamana ya wadhifa wa Makamu wa Rais katika uongozi wa nchi na Taifa letu ni ya Kikatiba kwa Mujibu wa Ibara ya 47 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Ibara ya 4(1) ya Katiba inafafanua kuhusu vyombo vyenye mamlaka ya nchi, kazi na mamlaka yake katika utendaji, kutekeleza utoaji haki na kutunga sheria na kusimamia utekelezaji katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ni kweli kuwa utaratibu wa kuwa na mgombea mwenza, unaozingatia umuhimu wa Rais na Makamu wa Rais kutoka chama kimoja cha siasa, ulirekebisha kule kuwa na Makamu wa Rais wawili na kubaki na mmoja tu.

Uhakika wa mfumo wa vyama vingi vya siasa unatamkwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 3(1) na nanukuu: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa." Ibara hiyo hiyo Ibara ndogo ya tatu imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Rais wa Jamhuri na Makamu wake, kwa wakati mmoja, hawatoki sehemu moja ya nchi mbili zilizoungana kuunda Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Ibara ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na napenda kunukuu: "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano." Tanzania si shirikisho. Tanzania Zanzibar kama ilivyokuwa Tanzania Bara, uwakilishi, kwa lugha ya Katiba, ni kupitia Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 66 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao tumebahatika na kupata fursa ya kuapa kuilinda, kuitetea na kuihifadhi, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vema na vizuri sana kujikumbusha kupitia Ibara hiyo, aina za Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , hususan Ibara ya 66 (1) inayosomeka na ninanukuu: "Bila ya kuathiri masharti mengine ya Ibara hii, kutakuwa na aina zifuatazo za Wabunge, yaani: -

(a) Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha Majimbo ya Uchaguzi.

(b) Wabunge Wanawake wa idadi inayoongezeka kuanzia asilimia 20 ya Wabunge waliotajwa katika aya ya (a), (c) na (d) itakayotajwa mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi kwa taarifa iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali baada ya kupata kibali cha Rais, watakaochaguliwa na Vyama vya Siasa vinavyowakilishwa Bungeni kwa mujibu wa Ibara ya 78 na kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo.

(c) Hapa ni muhimu sana Mheshimiwa Spika, Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa Wajumbe wake.

(d) Mwanasheria Mkuu.

(e) Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa kwa mujibu wa Ibara ya 67 isipokuwa sifa iliyotajwa katika Ibara ya 67(1)(b).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mwuliza swali ni Mjumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyechaguliwa kuwakilisha Jimbo la Uchaguzi la Jang'ombe lililoko Tanzania Zanzibar, nina hakika Mheshimiwa Mbunge wa Jang'ombe ni sehemu ya uwakilishi wa Zanzibar katika masuala ya Muungano. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa waasisi wa Muungano, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Abeid Amani Karume katika makubaliano ya msingi walikubaliana kwamba, Rais wa Zanzibar atakuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutokana na mabadiliko haya yaliyofanywa ya Katiba, Rais wa Zanzibar amekuwa hana nafasi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kutokupata heshima hasa pale anapotoka nje ya nchi, kinyume na pale ambapo Rais wa Zanzibar alipokuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, Serikali haioni mabadiliko haya yaliyofanywa yamemfanya Rais wa Zanzibar aonekane kama ni Waziri tu wa kawaida kinyume na yale makubaliano ya msingi?

**SPIKA:** Lakini swali hilo si lilijibiwa kwa ukamilifu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mkutano uliopita. Kwa hiyo, Kanuni haziruhusu liulizwe tena. Tuendelee na maswali mengine. Mheshimiwa Waziri, ni vema unaweza kuondoka kwa

sababu swali namba 22 mwenye kuliuliza ameliondoa. Kwa hiyo, tunakwenda swali namba 23.

Na. 22

**Malengo ya *TASAF***

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali)*

Na. 23

**Kero ya Maji - Arumeru Mashariki**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

Kwa kuwa upatikanaji wa maji umekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Arumeru Mashariki - Tarafa za King'ori hususan Ngabobo, IIkirimun, Karasi, Shiston, Kata ya King'ori, yenye wakazi 20,000, Mbuguni, Kata za Kikwe, Mbuguni, Makiba na Maroroni. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wakazi wa maeneo hayo kuhusu kero hiyo kubwa ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yana tatizo kubwa la kutokuwa na maji safi, salama na yasiyotosheleza mahitaji ya wananchi. Hata hivyo, Serikali imefanya juhudi mbalimbali kwa lengo la kutatua matatizo hayo kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na wananchi, imebuni Mradi wa *MAKELENA* katika Tarafa ya King'ori utakaohudumia Vijiji vya Ngabobo, Karasi, IIkirimun na Shiston. Chanzo cha maji cha mradi huu ni chemichemi zilizopo kwenye Mlima Meru. Mradi huo unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 120 utakapokamilika na utahudumia vijiji vinne nilivyovitaja. Mradi huu unatarajiwa kufadhiliwa na Shirika la *World Vision* kwa kushirikiana na Serikali. Serikali inaendelea kutafuta fedha kama mchango wake ili kutekeleza mradi huu.

(b) Katika Vijiji vya Mbuguni, Makiba na Maroroni, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya na kwa kushirikiana tena na Shirika la *World Vision,* hivi sasa inafanya ukarabati wa miradi ya maji ya Tuvaila/Maji ya Chai/Kikatiti/Samaria. Ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa mita 90 na ulazaji wa mabomba kutoka tanki hilo hadi tanki lingine la mita za ujazo 45, umekamilika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu inaendelea na matayarisho ya kupanua utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, unaofadhiliwa na mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa lengo la kuingiza Wilaya mpya 38 na kufanya jumla ya Wilaya zote nchini kuwa 50 chini ya mradi huu. Wilaya ya Arumeru ni mojawapo ya Wilaya 38 mpya zitakazonufaika. Mradi huo utaanza kutekelezwa mwaka ujao wa fedha. pamoja na jitihada hizo za Serikali, nawaomba wananchi waimarishe Kamati na Mifuko yao ya maji ili miradi hiyo iwe endelevu. Aidha, wananchi wajiandae kupokea na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mradi nilioutaja wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, waweke kipaumbele katika kuvipatia maji vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ili kuondokana na kero ya maji.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye matumaini. Swali dogo la nyongeza.

Mto Kikuletwa ambao ndiyo matumaini makubwa kwa maisha na maendeleo ya Tarafa ya Mbuguni na tangu mwaka 1946 haujawahi kukauka, wakati huu ninavyozungumza sasa hivi huo mto umekauka na ndiyo tegemeo kwa Tarafa nzima ya Mbuguni na Kaskazini mwa Wilaya ya Simanjiro.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Je, Wizara ipo tayari kusimamisha hatimiliki za maji katika mto huo ili kunusuru maji yanayofurika kwenye mto huo ili yaweze kwenda kwenye maeneo ya Mbuguni na Mikungani kwa ajili ya kumwagilia ili kunusuru mazao ya wananchi kwenye sehemu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kupungua kwa maji katika Mto Kikuletwa hakusababishwi na uchukuaji wa maji mengi katika mto huo ila tatizo kubwa ni kwamba, kumekuwepo na ukataji miti na uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa sana kwenye vyanzo vya mto huo, ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja. Lakini pia napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa vile wananchi wa Arumeru wameona tatizo hilo na nikishirikiana na Mheshimiwa Mbunge, jitihada zinafanyika ili kuwahamasisha kutokuendelea kuchafua vyanzo vya maji kwa kupanda miti. Ningependa nirudie kusema kwamba, kupungua kwa maji katika mto huo hakutokani na kuchukuliwa kwa maji, kama sababu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema, kwa hiyo, naomba tushirikiane kwenye hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margareth Bwana, kumbuka swali la msingi linahusu Kata ya King'ori.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Sambamba na swali la msingi na jitihada nzuri zinazofanywa na wananchi wetu kote nchini za kujenga shule za sekondari, moja

ya matatizo makubwa ambayo yanajitokeza katika maeneo hayo ni tatizo la maji. Nilikuwa napenda nifahamu kama kuna mkakati wowote maalumu wa Serikali kuhakikisha kwamba wanachimba visima katika maeneo hayo ya shule ili kumaliza tatizo hilo la maji katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nadhani kabla ya kuangalia matumizi ya maji kutoka kwenye visima virefu na vifupi kwa ajili ya shule zetu. Ningependa kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kuwahamasisha kwamba ujenzi wa shule unapofanyika sasa hivi tunapoezeka paa zetu ni vizuri tuanze kuvuna maji ya mvua. Paa za shule ni maeneo makubwa sana ambayo yanaweza kutupatia maji ya kutosheleza karibu nusu mwaka ya matumizi ya shuleni. Kwa hiyo, ningependa tuanze na hilo kabla hatujaanza kuangalia mbinu nyingine badala ya kuachia maji yanatiririka kwenye mito na kwenda kwenye bahari bila matumizi.

Na. 24

**Magonjwa ya Mifugo**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa alitoa Waraka Namba 1 wa mwaka 2002 kuhusiana na maagizo maalum ya namna ya kushughulikia magonjwa ya mifugo na kwa kuwa hadi sasa magonjwa ya mifugo yamekuwa yakiua mifugo mingi sana hapa nchini. Je, ni kwa nini hali hiyo inajitokeza pamoja na kuwepo kwa agizo muhimu la Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais alitoa Waraka Na. 1 wa mwaka 2002 kuhusu hatua za kuzuia kuenea kwa magonjwa ya Mifugo nchini, ambao umeainisha maeneo yatakayoshughulikiwa na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na wananchi. Hali ya kuendelea kuwepo kwa magonjwa nchini, licha ya Waraka huo muhimu, imetokana na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na Halmashauri nyingi kutokuwa na wataalamu wa mifugo wa kutosha ili kuweza kusimamia na kutekeleza Waraka huu na wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kutozingatia kikamilifu maelekezo yaliyomo katika Waraka unaotakiwa kusimamiwa na Halmashauri za Wilaya na Miji popote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maagizo ya Waraka huu, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) Serikali imeendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa kama vile Homa ya Mapafu ya ng'ombe. Hadi Desemba, 2003, jumla ya ng'ombe milioni 8 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa huu katika Wilaya 83 na zoezi linaendelea;

(ii) Serikali inafanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusu mifugo na mazao yake, ili ziweze kukidhi mahitaji ya soko huria. Kwa mfano, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo ya mwaka 2003, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu hivi karibuni, itasaidia sana kusimamia usafirishaji wa mifugo na udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Kanuni za sheria hii zinapigwa chapa hivi sasa na sheria itaanza kutumika hivi karibuni;

(iii) Serikali imeanzisha vituo 30 mipakani *(Border Posts)* ili kudhibiti mienendo ya mifugo inayoingia na kutoka nchini kwa lengo la kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini. Hii ni pamoja na ushirikishwaji wa sekta ya wanyamapori ili kudhibiti magonjwa yanayoweza kutokea kupitia wanyamapori na kuathiri mifugo;

(iv) Serikali imeanza kutoa ruzuku kwa Halmashauri za Wilaya na Miji kwa ajili ya kufufua majosho. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali imetoa shilingi 945,000,000 kwa ajili ya kukarabati majosho 199 katika Wilaya 59; na

(v) Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, inahamasisha wafugaji kuunda vikundi vya ushirika kwa lengo la kuendesha majosho ikiwa ni pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi kuendesha majosho hayo. Hadi sasa vipo vikundi 513 vya wafugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Waraka Na. 1 wa mwaka 2002 kuhusu hatua za kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini, yanategemea sana ushiriki wa wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Serikali itaendelea kushirikiana nao.

Napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie juhudi za Serikali katika kuhamasisha utekelezaji wa maagizo ya Waraka huu katika maeneo wanayotoka. Hii ni pamoja na Halmashauri za Wilaya kufungua mifuko ya maendeleo ya mifugo, kujenga vituo vya ukaguzi wa mifugo, majosho na vituo vya kutolea tiba za mifugo ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo hapa nchini.

**MHE JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

La kwanza, amezungumzia habari ya Mifuko ya Maendeleo ya Mifugo ambayo kwa kiwango kikubwa ilikuwa inategemea kupata asilimia fulani kutokana na kodi ya mifugo ambayo imefutwa na Serikali. Sasa je, mifuko hii itaendeshwaje, Serikali ina mpango wa kuweka chochote kwenye mifuko ile?

La pili, mpaka sasa ugonjwa pekee ambao Serikali inasaidia wafugaji ni ugonjwa wa homa ya mapafu ya mifugo, magonjwa mengine msaada sana sana haupo. Serikali inasema nini kuhusu kuwasaidia wafugaji katika magonjwa mengine zaidi ya huu wa homa ya mapafu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda ieleweke wazi kwamba, pale kodi mbalimbali za mifugo kama kodi ya mifugo ilipoondolewa Serikali kupitia Hazina na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatoa ruzuku moja kwa moja kufidia pengo la kodi hizo zilizofutwa. Sasa isieleweke kwamba, kodi kufutwa ndiyo mafungu hayo yamepotea moja kwa moja. Ni vizuri sisi Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani hapa nchini, kuzibana Halmashauri zetu, kwa sababu hakuna upotevu wowote unaotokana na kufutwa kwa kodi hizo. Serikali Kuu inafidia kwa kiwango kile kile walichokuwa wanakitumia na kukikusanya wakati kodi hizo zikiwepo.

La pili, kwa nini tunaangalia ugonjwa mmoja tu na magonjwa mengine hatuangalii. Ni kweli hii inatokana na kwamba fedha tunazopata kwa mapato mbalimbali ya Serikali zinahitajika kwa ajili ya shughuli nyingi. Hivyo basi, tunaangalia ugonjwa ambao una matatizo zaidi ya kuenea kwa haraka zaidi na kuua mifugo mingi ndiyo tunaweka nguvu zetu zote. Lakini wakati huo huo tunaomba Halmashauri za Wilaya, watu binafsi na wafugaji wenyewe, kushiriki katika kupiga vita magonjwa ya mifugo hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Idara za mifugo katika Mikoa hazina madawa au haziuzi madawa kwa hivi sasa. Je, Serikali inahakikishaje kwamba wafanya biashara wanayo madawa ambayo yanahitajika pindi milipuko ya magonjwa ya mifugo inapotokea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kama inavyoeleweka, ilijitoa katika shughuli ya uagizaji wamadawa. Lakini tunahamasisha sekta binafsi kuwa na uwezo mkubwa wa kuweka madawa ili yatumike yanakohitajika.

Sasa sekta binafsi kama inavyoeleweka, inakuwa *driven* na *demand. Demand* ikiwa kubwa *supply* itakuwepo. Lakini hata hivyo Serikali kwa kupitia mafungu ambayo nimeyasema katika jibu langu la msingi, tunajitahidi tunapopata fedha tunanunua madawa na chanjo na tunazipeleka kwenye Halmashauri ya Wilaya, ambapo tunahitaji wale wananchi wanaopata huduma waweze kuchangia kidogo ili kuendeleza mfuko huu wa ununuzi wa madawa na chanjo hapa nchini. Kwa hiyo, napenda niombe na kutoa rai kwa wananchi hasa wafanyabiashara kwamba, *demand* ya haya madawa ipo na hivyo wayaagize ili wananchi waweze kuyapata karibu na maeneo yao.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ugonjwa wa miguu na midomo ni ugonjwa sugu sana unaosababisha minada kufungwa kila wakati. Je, Serikali ina

utaratibu gani wa kutafuta dawa ya kinga kwa ajili ya mifugo ili wafugaji waweze kupata bei nzuri kwa mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, matatizo ya kuendelea kwa milipuko wa magonjwa hayo ya miguu na midomo inatokana na sababu moja kwamba, wananchi tunapokuwa na matatizo kwamba ugonjwa uko sehemu fulani badala ya kukimbilia kuchanja mifugo, tunaitoa kwenye maeneo hayo na kuipeleka kwenye maeneo mengine. Hivyo, jitihada zote za kuweza kuudhibiti ugonjwa inakuwa ni ngumu sana. Lakini chini ya sheria tuliyoipitisha mwaka 2003, kanuni zinatungwa ili kutaka kila mwenye mifugo aweze kuchanja mifugo yake inapoitishwa kuchanjwa kwa ajili ya ugonjwa fulani. Njia hiyo tu ndiyo itakayotusaidia ikiwa udhibiti wake utakuwa bora na ukisaidiwa sana na uongozi huko Wilayani. Kwa hiyo, bila kufanya hivyo itakuwa ni vigumu sana kwamba wananchi wanaochanja mifugo yao wataepuka lakini baada ya muda ugonjwa utarudi kwa sababu kuna baadhi yao hawakuchanja mifugo yao.

Na. 25

**Simba Wala Watu**

**MHE. BERNARD K. MEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Lindi hasa katika Wilaya ya Lindi Vijijini imepoteza watu zaidi ya hamsini kwa kuliwa na Simba; na kwa kuwa jitihada za kuwaua Simba hao zinakwama kutokana na kuwepo kwa misitu mingi; na kwa kuwa adui mkubwa wa mnyama huyo ni Mbwa Mwitu:-

(a) Je, Serikali iko tayari kupeleka kutoka Serengeti Mbwa mwitu 20 ili nao watusaidie kuwawinda na kuwala Simba hao?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa kifuta machozi kwa familia za watu walioliwa na wanyama hao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, kumekuwepo na matukio kadhaa ya Simba kula watu katika Wilaya ya Lindi Vijijini. Serikali kwa upande wake, imekuwa ikichukua hatua za kudhibiti tatizo hili ikiwa ni pamoja na kutuma Askari Wanyamapori kutoka Kikosi Dhidi Ujangili (KDU) kwenda kuungana na Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kuwasaka na kuwaua Simba wala watu kila tukio linapojitokeza. Mathalani katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2000/2001 - 2002/2003), Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, iliendesha msako wa Simba wala watu na kufanikiwa kuwaua Simba 8, chui 13 na fisi 11.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mheshimiwa Bernard Membe kuwa mbwa mwitu ni adui mkubwa wa Simba kwa maana kuwa anawala, haina uthibitisho wa kitaalam kwa vile kwa kawaida wanyama walao nyama hawali wanyama wenzao walao nyama. *(Makofi/Kicheko)*

Aidha, suala la kuwahamisha wanyapori wa aina yoyote wakiwemo mbwa mwitu kutoka sehemu wanayoishi na kuwapeleka katika eneo lingine jipya linahitaji kufanyika kwa uangalifu wa hali ya juu. Zoezi kama hili linahitaji maandalizi kwa kufanya utafiti wa kina ili kupata taarifa za uhakika na za kisayansi kuhusu athari zinazoweza kutokana na utekelezaji wake. Hatua hii ni muhimu kuwezeshwa kufanya maamuzi yaliyo sahihi. Mambo muhimu ya kutazamwa ni pamoja na yafuatayo:-

- Kuwa na takwimu sahihi ya idadi ya wanyama husika katika eneo wanakoishi na kujihakikishia kuwa idadi inayopendekezwa kuhamishwa haitaathiri kuzaliana kwa mnyama huyo huko anakotoka na kule anakopandikizwa.

- Kujua historia na upatikanaji wa mahitaji muhimu na ya msingi kama vile chakula, maficho/usalama na magonjwa hasa ya kuambukiza katika eneo la kuwahamishia.

- Kujua kama wanyama husika wana historia ya kuishi katika eneo hilo linalopendekezwa

- Kufanya tathmini ya kina ya athari kwa mazingira zinazoweza kutokea kutokana na kupandikizwa kwa wanyama katika eneo geni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hakuna ushahidi wa kisayansi kuwa mbwa mwitu ni adui wa Simba kama Mheshimiwa Mbunge wa Mtama anavyoeleza katika hoja yake, Wizara haioni kama kupeleka mbwa mwitu kwenye Wilaya ya Lindi Vijijini kutasaidia kudhibiti Simba katika eneo hilo na maeneo mengine yenye matatizo ya Simba. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara itaendelea kushirikiana na wananchi wa Wilaya hiyo na kwingineko, kusaka Simba na wanyama wengine waharibifu kwa lengo la kuwadhibiti.

Aidha, kuhusu kutoa kifuta machozi kwa familia za marehemu wanaoliwa na Simba, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara ina utaratibu wa kutoa kifuta machozi kwa kila familia inayofikwa na mkasa kama huo baada ya kupokea taarifa na uthibitisho wa kuwepo kwa tukio kama hilo.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Pamoja na hayo naomba nitoe nyongeza ya maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo la Simba hawa linajirudia rudia kila mara; na kwa kuwa Vijiji vinavyohusika bado vina wasi wasi kwamba tatizo hili litakuwa linajirudia; je, kama mbwa mwitu hawawezi kuifanya kazi ile tunaweza tukapata Morani wa Kimasai 20 wanaoweza kuja kutoa mafunzo kwa vijana wetu waliomaliza Mgambo ili na wao waweze kujihami kama wenzetu wanavyojihami?

Pili, Serikali sasa itakuwa tayari kuchukua ushauri wangu wa kuvipa upendeleo Vijiji vyote vikubwa ambavyo vina hatari ya mnyama huyu kwa kuvipatia silaha na mafunzo bora, waelekezwe tu namna ya kutunza silaha zile na maghala yale ili waweze kuwa na uwezo wa kujilinda wao wenyewe? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nina hakika kwamba, Morani wa Kimasai watafika huko baada ya Daraja la Mkapa kuwepo hivi sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini niseme kwamba, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, Maafisa Wanyamapori na Idara ya Wanyamapori pale ambapo tunapata matatizo mara moja tunapeleka watu wetu kwenda kudhibiti hali hiyo na kupeleka silaha pamoja na kwamba katika maeneo yale ambapo uwindaji wa kitalii asilimia 25 inapelekwa kwenye Halmashauri ambayo tunaamini fedha hizo pia zinatumika katika kununulia silaha hizo.

Kuhusu suala la upendeleo, tutaendelea kufanya kama vile tunavyofanya siku zote na naomba wananchi waelewe kwamba, Serikali inawajali sana. Lakini tumekuwa na wanyama hao ambao wapo siku zote na mara nyingine inawezekana kwamba, wananchi wanaweza kusogea maeneo ambayo wako wanyama. Lakini mara nyingine inatokezea pale ambapo kunakuwa na ukame, wanyama hawa huwa wanasogea maeneo haya. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutazidi kushirikiana.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona leo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa eneo hili lina misitu na wanyama wengi tu pamoja na tembo wanapatikana katika maeneo ya Lindi Vijijini ...

**MBUNGE FULANI:** Ndovu.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Ndovu sio tembo, haya. Simba, chui kama alivyoorodhesha. Je, haujafika wakati sasa kutafuta eneo ambalo litakuwa hifadhi ya wanyama katika Wilaya ya Lindi Vijijini ili wanyama hawa waswagwe wakusanywe katika eneo hilo badala ya kuzagazagaa hivi sasa Vijijini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuwaswaga wanyama hawa kwa kweli sio kama ng'ombe ambapo unawapeleka kwenye hifadhi. Ni wanyama ambao wanatembea kila sehemu. Hata wanyama ambao wapo kwenye Hifadhi za Taifa wanatoka kwenda katika maeneo mengine. Ndiyo maana kunakuwa na *corridors* mbalimbali au kwa Kiswahili wanaita shuruba katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, hili kwa kweli sio jibu. Nasema kwamba wanyama hawa wapo na *eco-systems* zetu ni budi wawepo wanyama pamoja na hiyo misitu. Kwa sababu pale unapokata misitu unakuwa na mashamba wanyama wanatokewa na wanaondoka. Kwa hiyo, kunakuwa na *eco-systems* ambazo zipo kwa mfano kama miti mirefu kwa ajili ya tembo na kadhalika. Hili nafikiri sio jibu lakini jibu kama nilivyosema awali ni kwamba, tutazidi kushirikiana na wananchi ili kuhakikisha pale ambapo panatokea matatizo basi Wizara inaingilia kati mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwanga kuna Simba. Eeh Mheshimiwa Maghembe, uliza swali. Simba wa Mwanga. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri alilotoa kwa swali la msingi. Lakini kwa kuwa wanyamapori wataendelea kuwa msingi mkubwa wa uchumi wetu hivi tunavyokwenda. Je, si wakati umefika sasa kwa Serikali au Mashirika ya Hifadhi ya Wanyamapori kuweka Bima kwa ajili ya kulinda mali na maisha ya wananchi badala ya kulipa kifuta machozi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, suala la Bima kwa kweli kwa wanyama wakali nafikiri halitoendana. Bima kwa kweli haziwekwi na Serikali siku zote, Bima inawekwa na wananchi. Kwa hiyo ni suala ambalo kwa kweli halipo kwanza katika Wizara yetu ni suala la Wizara ya Fedha. Lakini nafikiri kwamba, kuweka suala la Bima na wanyamapori halitoendana itakuwa ni ngumu sana.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba, hili halitowezekana kwa sababu wanyama hawana akili. Mara nyingi sana hawana akili wana-*charge* tu wanaumiza watu na kadhalika. Sasa sijui Bima ya kiasi gani ambayo italipwa, itakuwa ni fedha nyingi sana.

Na. 26

**Ndege Wanaohama Mahali Kwa Vipindi Fulani**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa habari zilizotolewa na gazeti la utafiti wa Shirika la *The Wildlife Society of Tanzania* katika miaka kadhaa iliyopita zinaonyesha kuwa wapo aina fulani ya ndege wanaohamia mahali kwa muda kila mwaka katika Maziwa ya Eyasi (Wilaya ya Ngorongoro) na Kitangiri (Wilaya ya Iramba) wakitokea Sweden na Siberia, Bahari ya *Antactic* - Ulaya katika miezi ya Novemba - Februari/Machi mwaka unaofuata wakati wa kipindi cha baridi kali huko Ulaya *(winter)*:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu ndege hao na kama kuna utafiti wowote uliofanyika kuhusu ndege hao ni nini kinachovutia ndege hao kuacha kuhamia kwenye maziwa mengine yote yaliyopo nchi nyingine za Afrika kama vile Afrika Kaskazini, Afrika Magharibi na Afrika ya Kati?

(b) Je, kama Serikali imefanya utafiti kutaka kujua ukweli wa viumbe hao ya kwamba ni kwa nini wanachagua kuhamia Maziwa ya Eyasi na Kitangiri, haioni kuwa hiyo ni raslimali muhimu na kivutio kwa shughuli za Utalii na Utafiti Kitaifa/Kimataifa na ni hatua gani ya kuhifadhi na kuboresha mazingira katika maziwa hayo ili ndege hao wazidi kupata hifadhi yao katika miaka ijayo?

(c) Je, kwa nini Serikali baada ya kufanya utafiti wa kutosha wa Maziwa hayo mawili ya Eyasi na Kitangiri wasitangaze kisheria kuwa ni hifadhi ya Taifa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Mashariki, naomba nitoe maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Serikali kujiunga na Mkataba wa Wanyamapori Wahamao *(Convention on Migratory Wild Animals - CMS)* na Mkataba wa Ndege Maji Wahamao kutoka Mabara ya Afrika, Asia na Ulaya *(African-Eurasian Water Birds Agreement - AEWA)* wa mwaka 1999.

Kuhusu Mkataba wa *AEWA* hadi sasa unajumuisha aina 235 za ndege ambao hutegemea Makazi ya ardhioevu *(Wetlands),* kikologia kama sehemu mojawapo ya mzunguko wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ndege wanaohamia Maziwa Kitangiri na Eyasi ni aina ya *Heroe.* Ndege hawa huvutiwa na upatikanaji na wingi wa chakula, makazi bora na ya usalama kwa mazalio na ukuzaji wa vifaranga. Idadi kubwa ya ndege hawa huzaliana hapa Tanzania. Ndege hawa mbali na kupatikana katika Maziwa ya Eyasi na Kitangiri, wanapatikana pia Kenya, Ethiopia, Botswana, Namibia, Senegal na Mauritania katika Bara la Afrika.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya utafiti wa ndege maji aina ya *Heroe*, hususan katika kuwahesabu ili kujua idadi yao. Utafiti ulifanyika mwezi Januari, 2002 na ulihusu kuhesabu ndege maji aina ya *Heroe (Flamingo)* katika maziwa ya magadi yakiwemo na Eyasi, Kitangiri, Manyara, Burunge, Natron, Empakai na Balangida. Vile vile, Wizara kwa ushirikiano na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi hususan Vyuo Vikuu, Taasisi za Utafiti na Sekretariati ya Mkataba wa Ndege Maji Wahamao Mabara ya Asia-Afrika-Ulaya, inafanya utafiti wa ufuatiliaji wa ndege hao ili kufahamu mwenendo wa maisha yao na maeneo wanayoyatumia katika mzunguko wa maisha yao. Matokeo ya utafiti huo yatatumika katika kupanga mipango ya hifadhi na matumizi endelevu.

(c) Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Mashariki, kwa kuona umuhimu wa kuhifadhi maeneo ya Eyasi na Kitangiri.

Taratibu za kutenga eneo kuwa eneo linalohifadhiwa kisheria, zinaanzia kwa wananchi waliopo kwenye maeneo hayo. Ni vizuri Mheshimiwa Shango, kwa kushirikiana na wananchi waliopo kwenye maeneo hayo wangeweza kutoa ridhaa yao, ili tathmini na taratibu za kufanya maeneo hayo kuwa maeneo yanayohifadhiwa kisheria ziweze kufanyika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeshaona umuhimu wa Bonde la Wembele-Eyasi na Kitangiri na sasa hivi Bonde la Wembele limeunganishwa kwenye mabonde nyeti ambayo yatahifadhiwa; na kwa kuwa *eco-system* ya Bonde la Wembele, Eyasi na Kitangiri ni moja yanalingana na lile la Ziwa Eyasi na Magadi; je, kwa kuwa wananchi wameitikia wito wa kutenga haya maeneo, Serikali sasa itashirikiana nao ili tupate hifadhi ya pekee inayohusisha haya maziwa mawili na tope la Wembele? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, ndio Serikali itashirikiana nayo. Lakini nimweleze kwa hivi sasa Serikali imeandaa programu ambayo kwa kushirikiana na Wizara yangu pamoja na *NEMC* na *Institute of Resources Assessment (IRA),* ambapo programu hii imepelekwa *GF* ili kuangalia ni jinsi gani ambapo tutapata fedha za kuweza kusimamia maeneo haya.

Na. 27

**Kutunga Sheria ya Ngono Haramu**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la maambukizi ya UKIMWI mwaka hadi mwaka; na kwa kuwa sababu kubwa inayochangia ongezeko hilo miongoni mwa sababu nyingi ni pamoja na vitendo vya ngono haramu zinazohusisha ukahaba, kujamiiana kwa watu wa jinsia moja na kinyume cha maumbile ya asili na uzembe:

Je, Serikali iko tayari kutunga Sheria ya Kuzuia kabisa vitendo vya ngono haramu vikiwemo vile vya usagaji na ushoga?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika nchi yetu kumekuwa na ongezeko la maambukizi ya Ugonjwa hatari wa UKIMWI mwaka hadi mwaka. Ni kweli pia kuwa moja ya sababu ya ongezeko hilo ni vitendo vya ukahaba. Wataalam wa mambo ya UKIMWI wanaona kwamba kujamiiana kwa watu wa jinsia moja hususan wanaume kwa wanaume ni moja ya njia inayoambukiza ugonjwa huu kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, tayari nchi yetu inayo sheria dhidi ya ngono haramu kama vile ukahaba, kujamiiana kwa watu wa jinsia moja na ngono kinyume cha maumbile. Sheria hiyo ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(Penal Code),* ambayo katika sehemu yake ya *XV* inayohusu makosa dhidi ya maadili *(Offences Against Morality)* imeainisha makosa ya kujamiiana na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tatizo la kuongezeka au kuendelea kwa makosa hayo si kwa kuwa hakuna sheria, bali ni tatizo ambalo linasababishwa na baadhi ya watu kutokuwa tayari kubadili mwenendo wa tabia zao kuhusu ngono haramu ikiwa ni pamoja na kuiga na kuendekeza tamaduni potofu za kigeni zinazoukubali ushoga na usagaji kwa kisingizio cha haki za binadamu. Licha ya kuwepo kwa sheria kali dhidi ya ngono haramu, kwa kiasi fulani imekuwa vigumu kudhibiti vitendo hivyo kwa kuwa kwa kawaida vitendo hivyo hufanyika kwa usiri mkubwa baina ya wahusika. Kuhusu kuongezeka kwa maambukizi ya Ugonjwa hatari wa UKIMWI, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, inajitayarisha kuandaa Muswada wa Sheria utakaosimamia udhibiti wa Ugonjwa wa UKIMWI, maambukizi na makosa yanayohusiana na ugonjwa huo. *(Makofi)*

**MHE MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sheria ipo lakini utekelezaji wake kama alivyosema Waziri ni mgumu, nafikiri inafanywa kwa siri sana watu hawaeleweki. Kwa hiyo, inaonyesha na Mahakama zetu zinashindwa kupata ushahidi wa moja kwa moja. Je, sasa taratibu gani zitakazotumika hadi kupunguza wimbi hili ili kuhakikisha kuwa hii hali inapungua na tunarudi kwenye mila zetu tulizoziacha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nadhani katika jibu langu la msingi nimekiri kwamba suala hili hutendeka kwa usiri mkubwa. Kwa hiyo, narudia tena kusema hivyo kwamba, kuna ugumu kuweza kubaini shughuli hizi zinavyotendeka. Hata humu ndani ya Bunge nadhani katika kipindi kilichopita kulikuwa kuna hisia hisia kwamba, kuna Wabunge fulani wanaendeleza ushoga, lakini sikuweza kupata ushahidi nikitegemea pengine ushahidi huu ningeupata kwa Mwenyekiti wetu wa Wanaume Mheshimiwa Edson Halinga. *(Makofi/Kicheko)*

Pia inasemekana kwamba mambo ya usagaji yalikuwa yakifanyika. Lakini pia sikuwa na ushahidi nilikuwa nataka nikutane na Mama Martha Wejja, anielimishe zaidi kuhusu hili. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 28

**Sheria ya Kuwalinda Wanawake na Watoto Wanaoathirika na Ubakaji**

**MHE. HAROUB S. MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imejitahidi kutunga sheria za kuwalinda Wanawake na Watoto na tunaipongeza Serikali kwa juhudi hizo, lakini kuna baadhi ya wakati Wanawake na Watoto ambao wameathirika na vitendo vya ubakaji kwa wakati tofauti tofauti

wamekuwa wakihojiwa na majina yao kutangazwa kwenye vyombo vya habari na kuzidi kuwadhalilisha:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja kutunga sheria ya kuwalinda waathirika hao?

(b) Kama sheria ya kuwalinda waathirika hao ipo, je, kuna chombo chochote cha habari kilichowahi kushtakiwa kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, tunashukuru na kufarijika kuona kwamba, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, ametambua juhudi zinazofanywa na Serikali, kutunga sheria ya kulinda Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari inayo Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 *(Sexual Offences (Special Provisions) Act, 1998),* ambayo pamoja na mambo mengine, inawalinda watoto na Wanawake walioathirika na vitendo vya ubakaji wasidhalilike zaidi. Kwa mfano, fungu la 28 la Sheria hiyo limefanya marekebisho katika fungu la 3 la Sheria ya Watoto na Vijana wa Umri Mdogo *(The Children and Young Persons Ordinance Cap. 13),* ambalo sasa linatamka kwamba watoto wote walio chini ya umri wa miaka 18, mashtaka yao yawe yanaendeshwa kwa faragha *(in camera)* na kama ushahidi wao inabidi utolewe kwa faragha. Vile vile fungu la 24 la Sheria hiyo ya Makosa ya Kujamiiana, ambayo imerekebisha fungu la 186(3) la Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985, linatamka kwamba, ushahidi unaotolewa kwa makosa yanayotokana na mambo ya kujamiiana unatakiwa utolewe kwa faragha na ushahidi huo na majina ya wahusika havitatakiwa kuchapishwa kwenye gazeti lolote au chombo chochote cha habari. Lakini sheria hiyo haizuii kuchapishwa au kuandikwa kwa jambo lenyewe hilo kwenye *Law Reports* au magazeti ya kitaaluma kwa nia ya kusambazwa kwa watu maalum katika masuala ya sheria au Madaktari kwa ajili ya wataalam wanaohusika na masuala ya madawa, kinga au uganga.

Hata hivyo, kwa mujibu wa maadili ya uandishi na utangazaji wa habari za aina hiyo, habari hizo zikichapishwa katika vyombo vya habari, jina na hata sura ya mhusika, havichapishwi katika habari hiyo na endapo picha hizo zitachapishwa, basi Mwandishi atatakiwa kuficha sura ya mhusika ili asiweze kujulikana na jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari ipo sheria inayowalinda Wanawake na Watoto walioathirika na vitendo vya ubakaji, Serikali kwa sasa haioni haja ya kutungwa sheria nyingine itakayosimamia makosa ambayo tayari yanasimamiwa na sheria nyingine iliyopo iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hatuna taarifa za kuwepo kwa chombo chochote cha habari kilichowahi kushtakiwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kuhusiana na kuwahoji na kutangaza majina ya waathirika wa vitendo vya ubakaji kinyume cha matakwa ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub, naomba ukubali tutoe nafasi kwa swali la mwisho, nyongeza yako uihifadhi. Nashukuru sana.

Na. 29

**Uuzaji na Utumiaji Mirungi**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza: -

Kwa kuwa uuzaji na utumiaji wa mirungi nchini Tanzania ni kinyume cha sheria za nchi na kwa kuwa mirungi ni kileo chepesi ikilinganishwa na vileo vingine vya Kihindi kama *Kuber, Manikachhand, Tulsi, Tambuu, Parik, Wariale, Chatini, Rasi, Popoo, Toplo* na *Dana:* -

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kupiga marufuku uingizaji na uuzaji wa *Kuber* na *Tulsi* ambazo hazina tofauti na madawa ya kulevya?

(b) Je, Serikali inasemaje juu ya ushirikiano wetu na nchi ya Kenya kibiashara ambapo Kenya imehalalisha matumizi na biashara ya mirungi?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya udhibiti na matumizi ya madawa ya kulevya katika baadhi ya mitaa yetu ya mijini na vijijini hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John E. Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imekuwa ikipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu kuwa *Kuber* na *Tulsi* zina kemikali zinazolevya. Baada ya kupata malalamiko hayo, Serikali imechukua hatua ya kupeleka sampuli za bidhaa hizo kwa Mkemia Mkuu kwa ajili ya uchunguzi wa kitaalam ili kuona kama zina kemikali zilizoko katika madawa ya kulevya. Matokeo ya uchunguzi umebaini kuwa *Kuber* na *Tulsi* havina madhara makubwa kwa binadamu anayetumia isipokuwa vina *nicotine* ya kawaida kama ilivyo kwenye sigara. Hivyo, Serikali haioni sababu ya kupiga marufuku matumizi ya vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, mirungi imo katika kundi la mimea yenye kemikali za madawa ya kulevya na madhara yake ni pamoja na kuharibu akili, kukosesha usingizi, kusababisha magonjwa ya moyo, kujisikia vibaya, kupunguza hamu ya kufanya mapenzi na kadhalika. Kwa sababu hizo mirungi imepigwa marufuku nchini mwetu na

Serikali inachukua hatua za dhati katika kupambana na wasafirishaji, wauzaji na watumiaji wa mirungi.

(b) Aidha, kwa kuwa baadhi ya mirungi inayotumiwa hapa nchini inaingizwa kinyemela kutoka nchi ya Kenya, Serikali inaendelea na jitihada zake za kuishawishi nchi hiyo, iharamishe uuzaji na utumiaji wa mirungi ili tuweke nguvu za pamoja za kupambana na madawa ya kulevya pamoja na mirungi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kupiga vita matumizi ya madawa ya kulevya hapa nchini. Katika kuimarisha mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, kimeundwa Kitengo vya Kuzuia Madawa ya Kulevya ndani ya Jeshi la Polisi na pia imeundwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa lengo la kusimamia na kuratibu vita hii. Aidha, Jeshi la Polisi limekuwa likifanya operesheni za mara kwa mara nchini kote, kukamata waingizaji, wauzaji na watumiaji wa madawa ya kulevya. Mapambano dhidi ya madawa haya yamekuwa yenye ufanisi mkubwa, kwa mfano, mwaka 2003/2004, Jeshi la Polisi limekamata kilo 5.8 za *heroine*, kilo 12,002 za mirungi na kilo 733,222 za bhangi kutoka mashambani. Wote waliohusika wamefikishwa mbele ya sheria na mapambano yanaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Singo, naomba usamehe haki yako ya kuuliza swali la nyongeza kwa sababu muda wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja tu la kikao ambacho siyo cha Kamati, lakini nimeombwa na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar kwamba, wakutane leo mara tu baada ya kikao cha asubuhi. Siyo sasa hivi, lakini ni baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi wakutane kwenye chumba namba 428.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili ni kwamba, mtakuwa mmeona leo kamera za *TV* zimeongezeka humu ndani, hii nyingine iko juu na hapa ziko nyingi na huku ipo nyingine. Kama nilivyowaarifu mapema hizi ni kamera za *STAR TV* kwa ajili ya kurusha matangazo moja kwa moja kutoka hapa ukumbini. Mmiliki wa *STAR TV* ameniambia kwamba, kulikuwa na tatizo la mawasiliano baina ya *satellite* na kituo cha urushaji matangazo kilichoko Mwanza, kwa hiyo, haikuwezekana kurusha moja kwa moja asubuhi hii, lakini anasema kuanzia saa 5.00 pengine mawasiliano yatakamilika. Kwa hiyo, yaliyotokea asubuhi hii yatakwenda kwenye mtandao wa *STAR TV.*

**MBUNGE FULANI:** Mmiliki wa *STAR TV* ni nani?

**SPIKA:** Mmiliki wa *STAR TV* ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo. Katibu, tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2004/2005

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka wa 2003 na Mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 - 2006/2007. Pamoja na Hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2003 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa mchango mkubwa ilioutoa wakati ikijadili muhtasari wa hotuba hii ambao umetuwezesha kuboresha kazi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani zangu kwa viongozi na wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa, Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi, ambao kwa ushirikiano wao na Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, chini ya Dr. Enos Bukuku, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Omar Bendera, kwa kufanikisha maandalizi ya taarifa hii na Mpango wa Muda wa Kati ninaouwasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kupata Ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi kule Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote, Viongozi wa Chama na Serikali, wapigakura wangu wa Handeni, ndugu, majirani na marafiki, kwa rambirambi zao na ushiriki wao katika mazishi ya marehemu baba yangu mpendwa, Mzee Omar Mohammed Kigoda, kule Handeni. Ahsanteni sana. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imekuwa ikitunga sera na kujiwekea mikakati na malengo katika maeneo na Sekta mbalimbali ili kuleta ufanisi katika utendaji wa shughuli zake ambazo ni pamoja na: -

- Katika Sekta ya Fedha, sera za kifedha zilizotungwa zimedhibiti ongezeko la ujazi wa fedha na kasi ya upandaji bei.

- Katika Bajeti ya Serikali, hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali zimeongeza ufanisi na kuhimiza nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali na kuongeza ukusanyaji mapato.

- Katika Sekta ya Biashara ya Ndani na Nje, mikakati ililenga kuondoa vikwazo na urasimu ili kutoa nafasi ya ushindani unaochochea ufanisi katika uzalishaji na utoaji huduma. Vile vile, Serikali ilitayarisha na kutekeleza mkakati wa kukuza mauzo nje ambao hadi sasa umeonyesha mafanikio.

- Katika Sekta Binafsi, sera na mkakati vimeendelea kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji binafsi kuwekeza katika Sekta mbalimbali za uzalishaji, utoaji huduma na ujenzi wa miundombinu.

- Katika Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Serikali imeendelea kufanya marekebisho kwa kutoa hisa kwa Sekta Binafsi, kuingia ubia, kubadilisha miundo na kufilisi yale yanayoleta hasara ili kuboresha ufanisi katika uendeshaji wa uchumi kwa jumla na kuondoa mzigo wa kuendelea kutoa ruzuku kutoka kwenye Bajeti ya Serikali.

- Katika Sekta ya Umma, muundo wa Serikali umefanyiwa tathmini na marekebisho kwa nia ya kuainisha upya majukumu ya Serikali, kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi. Serikali Kuu imekasimu baadhi ya madaraka yake kwa Serikali za Mitaa ili kuwapa Wananchi uwezo wa kupanga na kutekeleza mipango na mikakati yao inayolenga katika kuondoa umaskini nchini.

Aidha, Serikali imetunga na kutekeleza sera mbalimbali za uchumi jumla na za kisekta na kuboresha sheria, hatua zote hizo zikilenga katika kuleta mageuzi katika mfumo wa uendeshaji uchumi, kukuza maendeleo ya jamii, kuimarisha utawala bora na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utekelezaji wa mikakati mbalimbali umeliwezesha Taifa kukuza uchumi, kutoa nafasi kwa Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi, kujenga mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji, kuvutia watalii, kuongeza nafasi za ajira, kuongeza mauzo nje, kuwezesha Wananchi kushiriki katika kuleta maendeleo yao na kuwezesha Taifa kuratibu na kusimamia uchumi wa soko.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio haya yanayotia moyo, uchambuzi wa mwenendo wa vigezo vya uchumi unaonyesha kwamba bado uchumi wetu unakabiliwa na changamoto nyingi ili kufikia shabaha kuu ya kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2015. Baadhi ya changamoto ambazo niliwahi kuzitaja ni pamoja na uchumi tegemezi, ukuaji mdogo wa uchumi unaotokana na uzalishaji mdogo katika Sekta ya Kilimo, miundombinu hafifu, ushindani dhaifu wa bidhaa zetu katika masoko ya nje, uwiano mdogo kati ya uwekezaji raslimali na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na vikwazo mbalimbali katika kushinda vita dhidi ya umaskini, kujenga uchumi imara unaokua kwa kasi na kuleta maendeleo

endelevu, pamoja na kuzingatia masuala mengine ya kimsingi, hapana budi kila Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Wizara, kuongozwa na dira, sera, mikakati na malengo ya muda wa kati na mfupi yanayojulikana na kutekelezeka katika Sekta ya Uzalishaji Mali hususan kilimo, Sekta ya Huduma za Kiuchumi na katika Sekta zitoazo huduma za kijamii. Aidha, mikakati ya utekelezaji izingatie upatikanaji wa mafanikio ya haraka, yaliyo endelevu na yaliyo katika kipindi cha muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, shabaha kuu ya Mpango na Bajeti ilikuwa ni kutekeleza mkakati wa kupunguza umaskini, kuendeleza mafanikio ya uchumi jumla yaliyopatikana hadi sasa, kukuza Sekta Binafsi na kuimarisha Serikali za Mitaa kwa kuzipatia madaraka na raslimali zaidi. Ili kufikia shabaha zetu kuu, malengo ya uchumi jumla kwa kipindi cha 2003/2004 - 2005/2006 ni kama ifuatavyo: -

- Pato la Taifa halisi kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2003, asilimia 6.6 mwaka 2004, asilimia 7.0 mwaka 2005 na asilimia 7.4 mwaka 2006;

- Kasi ya upandaji bei kupungua hadi asilimia 4.0 ifikapo Juni, 2004, baadaye kupungua kulingana na viwango vitakavyokuwepo katika nchi tunazofanya nazo biashara kubwa;

- Kuongeza mapato ya ndani kufikia uwiano na Pato la Taifa kwa bei husika kwa asilimia 13.2 mwaka 2003/2004, asilimia 13.5 mwaka 2004/2005 na asilimia 13.7 mwaka 2005/2006; na

- Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ($M_2$) linalowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei na kuwa na akiba ya fedha za kigeni ya kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mwenendo wa Uchumi na Bajeti katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 umeonyesha sura ya mchanganyiko. Ukosefu wa mvua katika sehemu kubwa ya nchi umesababisha uzalishaji kupungua katika Sekta ya Kilimo hususan mazao na mifugo, hali ambayo ilisababisha uhaba mkubwa wa chakula katika Mikoa mingi hapa nchini. Licha ya ukame uliojitokeza, hali ya uchumi kwa ujumla na mwenendo wa Bajeti ya Serikali havikuathirika sana. Ukuaji wa uchumi kwa jumla uliendelea kuwa imara, kasi ya upandaji bei imebakia chini ya asilimia 5.0 na akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia uwezo wa kuagiza bidhaa na malipo ya huduma kwa zaidi ya miezi nane na nusu. Takwimu zinaonyesha kuwa uchumi ulikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2003 ikilinganishwa na lengo la asilimia 6.3. Lengo halikufikiwa kutokana hasa na kupungua kwa ukuaji katika Sekta ya Kilimo uliokua kwa asilimia 4.0 mwaka 2003. Hata hivyo, baadhi ya Sekta hususan viwanda, biashara (inayojumuisha utalii), madini, usafiri, mawasiliano na fedha, zilikua kwa viwango vya kuridhisha katika mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha mwaka 2003 kasi ya upandaji bei iliendelea kuwa chini ya asilimia 5. Katika mwezi wa Februari kasi ya upandaji bei ilifikia kiwango cha chini kabisa cha asilimia 4.2. Hata hivyo, kipindi cha kuanzia Aprili,

2003, kasi ya upandaji bei ilianza kuongezeka kidogo kidogo hadi kufikia asilimia 4.6 Desemba, 2003, kiwango ambacho kimeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 6.5 Aprili, 2004. Wastani wa kasi ya upandaji bei kwa mwaka 2003 ulikuwa ni asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2002. Ongezeko la kasi ya upandaji bei linatokana hasa na kuongezeka kwa bei ya vyakula. Vile vile ongezeko la bei za mafuta ya petroli zimechangia katika kasi ya upandaji bei za bidhaa nyingine. Kutokana na dalili nzuri ya upatikanaji wa chakula katika baadhi ya Mikoa, matarajio ni kwamba, kasi ya upandaji bei itashuka na kufikia asilimia 4.0 ifikapo Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ($M_2$) ulipungua kutoka asilimia 20.7 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 14.1 mwaka 2003. Kutokana na udhibiti huu, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ($M_2$) , umekuwa ndani ya wastani unaolengwa ambao ni kati ya asilimia 12.0 na 15.0. Kupungua kwa kasi ya ujazi wa fedha kumetokana na juhudi za Benki Kuu kufuatilia kwa nia ya kutengamaza ujazi wa fedha unaoendana na malengo ya ukuaji wa uchumi.

Katika kipindi cha mwaka 2003 mikopo iliyotolewa kwa Sekta Binafsi iliongezeka kwa asilimia 43.2. Hivyo, mchango wa mikopo iliyotolewa na Benki za Biashara kwa Sekta Binafsi uliongezeka kutoka asilimia 68.4 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 98.4 ya mikopo yote katika mwaka 2003. Kuongezeka kwa mikopo kwa Sekta Binafsi kulitokana na shughuli za kibenki na kuongezeka kwa mikopo midogo midogo *(micro-finance)* iliyotolewa kwa shughuli za uzalishaji mali na biashara ndogo ndogo vijijini na mijini. Aidha, katika mwaka 2003 mchango wa mikopo ya Benki za Biashara kwa Bajeti ya Serikali umepungua kutoka asilimia 31.6 mwaka 2002 hadi asilimia 1.6 kupungua kwa mikopo kwa Sekta ya Umma kunatokana na azma ya Serikali kufuatilia utekelezaji wa sera yake ya kutaka Mabenki na Vyombo vya Fedha nchini kuelekeza mikopo zaidi kwa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, thamani ya fedha ya Tanzania kwa mwaka 2003 ilikuwa ni wastani wa Shilingi 1,038.6 kwa Dola moja ya Kimarekani ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 966.6 kwa Dola moja ya Kimarekani mwaka 2002. Hii inaonyesha kuwa sarafu yetu inaendelea kupungua thamani mwaka hadi mwaka na hivyo kufikia upungufu wa wastani wa asilimia 7.4 kwa mwaka 2003. Kupungua kwa thamani ya Shilingi kulichangiwa hasa na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kulikosababishwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa. Mojawapo ya njia za kuongeza thamani ya Shilingi ni kuongeza kasi ya mauzo nje. Licha ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuongezeka hadi kufikia wastani wa Shilingi 108 bilioni kwa mwezi, bado uwiano kati ya mapato ya ndani na Pato la Taifa ni mdogo. Matarajio ya Serikali hadi Juni, 2004 ni kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua Shilingi 1,342 bilioni sawa na asilimia 12.8 ya Pato la Taifa. Kwa kadri uchumi unavyokua na kuboreka, lengo la Serikali ni kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka lengo la asilimia 15.1 kwa mwaka 2004/2005 hadi asilimia 16 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi kama ilivyokuwa mwaka 2002/2003, Serikali iliendelea kuelekeza matumizi makubwa katika Sekta zinazopewa kipaumbele chini ya mkakati wa kupunguza umaskini. Hata hivyo, hali ya ukame

imesababisha matumizi makubwa kuliko yalivyotarajiwa katika Sekta ya Nishati na ununuzi wa chakula. Matumizi hayo yamesaidia kupunguza makali ambayo yangetokea katika uchumi iwapo Serikali isingechukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwishoni mwa Desemba, 2003 deni la Taifa linalojumuisha deni la nje na ndani lilifikia dola za Kimarekani 8,755.0 milioni. Kati ya fedha hizo dola 7,890.7 milioni au asilimia 90.1 ya deni lote ni deni la nje na dola 864.3 milioni au asilimia 9.9 ni deni la ndani. Kuongezeka kwa deni la Taifa kumetokana na kumetokana na kupokelewa kwa mikopo mipya pamoja na malikizo yatokanayo na madeni ambayo hayajasamehewa na nchi zisizokuwa wanachama wa Klabu ya Paris. Serikali iliendelea kubadilisha madeni yake ya ndani katika dhamana zisizouzika *(Government Securities)* ili kurefusha kipindi cha kulipia madeni yake na hivyo kupunguza mzigo wa deni hilo katika bajeti yake ya mwaka na kuingiza dhamana na hatifungani *(bonds)* hizo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kusamehewa madeni kutoka taasisi za fedha za Kimataifa *(IMF* na *ADB)* na wanachama wa Klabu ya Paris, waliotoa unafuu kwa kufuta hadi asilimia 90 ya deni lote kwa thamani halisi. Hata hivyo Serikali inaendelea kushauriana na nchi zisizo wanachama wa Klabu ya Paris, ili nao wakubali kutufutia madeni kwa kutumia utaratibu wa vigezo vya wanachama wa Klabu ya Paris. Hadi Desemba, 2003 jumla ya madeni yaliyofutwa chini ya mpango wa *HIPC* yalifikia dola za Kimarekani 749.7 milioni. Nchi zisizokuwa wanachama wa Klabu ya Paris, ambazo zilitoa unafuu kwa njia ya kufuta madeni ni pamoja na China, Bulgaria, India na Kuwait ambao walisogeza mbele muda wa kulipwa deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa nje imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kuashiria mwenendo mzuri wa biashara. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 26.6 kutoka dola 902.5 milioni mwaka 2002 na kufikia dola 1,142.4 milioni mwaka 2003. Ongezeko hilo la thamani lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia, sehemu kubwa ikiwa ni madini na hasa dhababu.

Aidha mauzo ya bidhaa asilia nayo yalichangia asilimia 19.5 baada ya kuongezeka kwa kiasi kilichouzwa nje pamoja na kuboreka kwa bei ya baadhi ya bidhaa katika soko la dunia. Thamani ya bidhaa *(f.o.b)* zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 30.5 na kufikia dola 1,973.0 milioni mwaka 2003 kutoka dola 1,511.3 milioni zilizoagizwa mwaka 2002. Kuongezeka kwa uagizaji bidhaa nje kumetokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya madini, ufufuaji wa sekta ya viwanda na uagizaji wa chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka mauzo ya bidhaa nje, bado kasi ya ukuaji wake haijafikia kiwango cha kulipia bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na hivyo kusababisha urari wa biashara ya bidhaa kuwa na nakisi ya dola 830.6 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola 608.7 milioni mwaka 2002. Nakisi hiyo imetokana na kuongezeka kwa uagizaji wa mafuta ya petroli, mitambo, malighafi za viwanda, vifaa vya

usafirishaji, vifaa vya ujenzi na chakula. Njia kuu ya kufuta nakisi hiyo ni kuongeza mauzo nje kwa kasi zaidi na kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 Serikali iliendelea na jitihada za kukuza mauzo ya bidhaa nje kwa kuendeleza mkakati wa *EPZ.* Kufikia mwezi Aprili, 2004 kiasi cha mitaji ya dola za Marekani 60.9 milioni ilikuwa imewekezwa, ambapo dola 48.5 milioni zilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya *NIDA Textile Mills, Millenium Business Park* na *Quality Industrial Park* yaliyoko jijini Dar es Salaam na dola 12.4 milioni zilikuwa ni kwa ajili ya uendeshaji katika kiwanda cha *NIDA* kilichoko Tabata, *Star Apparels (T)* na *Reclaimed Appliances (T)* vilivyoko *Ubungo Millennium Business Park.* Viwanda hivi kwa sasa vimeanza uzalishaji na kukuza bidhaa zake nje. Aidha, zoezi la kutathmini na kautoa leseni za uendeshaji katika maeneo mengine zaidi kwa ajili ya mkakati wa *EPZ* linaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza kasi ya mauzo nje tumeendelea pia kutumia fursa mbalimbali za ushirikiano wa kikanda na kimataifa kama vile mpango wa *AGOA* na mpango wa *Everything But Arms(EBA)* na fursa nyinginezo ambazo zinatoa nafasi ya kuuza bidhaa kwa masharti nafuu ya kodi au bila ya kuwekewa kodi yeyote. Hata hivyo bado hatujaweza kutumia fursa hizi kwa ufanisi kama wenzetu katika nchi jirani wanavyofanya. Tatizo linalotukwamisha ni pamoja na kutokuwa na uzalishaji wa bidhaa nyingi na bora, miundombinu hafifu na ujuzi mdogo wa masoko ya ujasirimali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kwa hali ya wasiwasi na vita hususan migogora ya kisiasa Mashariki ya Kati, katika mwaka 2003 Pato la dunia lilikua kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2002. Pato la nchi zilizoendelea lilikua kwa asilimia 2.1 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2002. Kwa nchi zinazoendelea Pato lilikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2003 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2002.

Aidha, pamoja na kukumbwa na matatizo ya magonjwa, ukame, migogoro ya kisiasa na maradhi, bado Pato la Afrika kwa mwaka 2003 lilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa ukuaji wa uchumi duniani kwa kipindi cha muda mfupi ujao unatia matumaini hasa ukizingatiwa ukuaji uliokuwepo kwa kipindi cha kuishia mwaka 2003 ambapo uchumi ulikua kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko kile kilichokuwa kimetarajiwa. Hata hivyo, matarajio hayo ya ukuaji wa uchumi duniani yanaweza kuathiriwa na kasi ya upandaji mkubwa wa bei za mfuta ya petroli, kuongezeka kwa tatizo la ugaidi wa Kimataifa na kutotengemaa kwa hali ya kisiasa katika eneo la Mashariki ya Kati. Athari za matatizo haya zimeanza kujitokeza sehemu nyingi duniani na hapa nchini kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na huduma za usafiri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliendelea kutekeleza mkakati wa maendeleo wa miaka mitano (2001 - 2005) kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kutekeleza programu zilizopewa kipaumbele kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa utekelezaji.

Aidha, juhudi zilielekezwa katika kukamilisha itifaki ya ushuru wa pamoja wa forodha ambayo hatimaye ilisainiwa mwezi Machi, 2004 Mjini Arusha, kwa lengo la kuimarisha bidhaa, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kuvutia wawekezaji kutoka nje na kukuza uchumi wa nchi za Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu yaliyokamilika katika itifaki hiyo ni pamoja na uondoaji wa ushuru wa bidhaa kwa biashara za ndani na utaratibu wa kuhakiki uasili wa bidhaa, uanzishaji wa mfumo mmoja wa ushuru wa forodha ambapo viwango vilivyokubaliwa ni kutotoza kodi kwa uagizaji malighafi, asilimia 10 kwa bidhaa za kati na asilimia 25 kwa bidhaa zilizokamilika. Vile vile, katika kuendeleza miradi ya pamoja nchi wanachama zilikubaliana kutoa kipaumbele kwa sekta ya barabara, nishati na uendelezaji wa Bonde la Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 Tanzania ilikuwa Mwenyekiti na mwenyeji wa mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC* uliofanyika Dar es Salaam mwezi Agosti, 2003. Wakuu wa Nchi na Serikali, waliidhinisha kuanza kutekelezwa kwa Mpango wa Mkakati wa Maendeleo *(Regional Indicative Strategic Development Plan - RISDP)* wa ushirikiano kwa kipindi cha miaka kumi na mitano ijayo kama dira ya ushirikiano katika sekta zote za Jumuiya.

Vile vile, nchi wanachama wa *SADC* zilisaini Mkataba wa Ulinzi na Usalama kwa lengo la kudumisha uhusiano na kuunganisha nguvu za utekelezaji wa malengo yaliyowekwa, kama moja ya misingi imara katika suala zima la ushirikiano kikanda na katika Bara la Afrika kwa ujumla. Hali ya kisiasa katika umoja wa nchi za *SADC* ilizidi kuimarika katika mwaka 2003 kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa amani nchini Angola na kusimikwa madarakani kwa Serikali ya mpito katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwezi Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizochukuliwa na nchi wanachama wa *SADC* za kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya kijamii na kikanda, bado changamoto kubwa hususan tatizo la ukame, mafuriko, ukosefu wa amani ya kudumu katika baadhi ya nchi wanachama pamoja na magonjwa kama vile Ukimwi, Malaria na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Katika azma ya kupambana na tatizo la ukame na ukosefu wa chakula, Wakuu wa Nchi za *SADC* walikutana mwezi Mei, 2004 Jijini Dar es Salaam na kuweka mkakati wa kuondoa ttizo hilo sugu kuwa endelevu.

Katika mkutano wa pili wa Umoja wa Afrika *(African Union)* uliofanyika Maputo, Msumbiji mwezi Julai, 2003 viongozi wa Afrika walikubaliana kuendelea kutekeleza malengo ya *NEPAD* ili kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Bara la Afrika. Hadi kufikia Desemba, 2003 nchi 15 za Afrika zilikuwa zimejiunga na utaratibu unaotoa fursa kwa nchi kufanyiwa ukaguzi na kupimwa ufanisi wake katika kutekeleza vigezo vya uchumi na utawala bora *(NEPAD Peer Review Mechanism).* Mpango huo unasisitiza uimarishaji na uzingatiaji wa masuala ya uwazi, utawala bora, kuheshimu haki za binadamu na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa uchumi.

Vile vile Wakuu wa Nchi na Serikali wa Ukanda wa Mashariki ya Afrika walikutana Mjini Nairobi, Kenya mwezi Oktoba, 2003 ili kujadili, kuchambua na kukubaliana kuhusu vigezo vya programu na miradi ya kupewa kipaumbele chini ya mpango wa *NEPAD* utaratibu wa kuratibu programu na miradi ya kikanda na jinsi ya kushirikisha sekta binafsi kwenye utekelezaji wa mpango wa *NEPAD*. Ili kuongeza ufanisi katika kuratibu programu na miradi ya kimaendeleo katika ukanda wa mashariki ya Afrika Wakuu wa Nchi waliridhia nchi ya Kenya kuwa mratibu wa programu na miradi ya kimaendeleo kikanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Serikali iliendelea na hatua mbalimbali zinazolenga katika kukuza uwekezaji rasilimali nchini. Kati ya hatua hizo ni pamoja na kukiwezesha Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* kuongeza ufanisi katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Jitihada hizi zimewezesha kituo kusajili miradi 372 yenye thamani ya shs. 1669.5 bilioni (sawa na dola za Kimarekani bilioni 1.6). Kati yake, miradi 229 ilikuwa mipya na 143 ilikuwa ni ya kupanua na kukarabati viwanda. Miradi 155 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani na miradi 109 ya wawekezaji wa nje na miradi 108 ilikuwa ya ubia. Aidha, mitaji ya kigeni ya moja kwa moja *(Foreign Direct Investments)* iliongezeka kufikia dola 300 milioni ikilinganishwa na dola 240.4 milioni mwaka 2002. Miradi hii inakadiriwa kutoa ajira kwa watu 198,458.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Baraza la Taifa la Biashara la Tanzania *(Tanzania National Business Council - TNBC)* zilikamilisha shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya mapitio ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 na kutoa ushauri kuhusu sheria mpya ya kodi ya mapato iliyopitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2004 na inayoendana na hali ya sasa ya biashara.

(ii) Kutoa ushauri kuhusu marekebisho ya sheria ya leseni za biashara ili kuondoa urasimu na kero katika taratibu za kupata leseni za biashara.

(iii) Kuanzishwa kwa kitengo cha *Better Regulation Unit(BRU)* kinachoratibu programu inayolenga kuboresha mazingira ya sekta binafsi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005 Serikali itaendelea na juhudi zake za kuimarisha mazingira na taratibu za kuvutia wawekezaji ili kuongeza uwekezaji rasilimali kwa kuanzisha midahalo ijulikanayo kama *Smart Partnership Dialogue* baina ya Sekta za Umma na binafsi. Lengo ni kuhamasisha na kuwezesha shughuli ndogo ndogo za uzalishaji na biashara kupata mikopo, wabia na teknolojia kutoka nje na ndani.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zitaanzisha mfuko ujulikanao kama *Chief Executive Scholarship Fund* kuongeza viwango vya elimu na ujuzi kwa watendaji katika sekta binafsi na sekta ya umma. Aidha, Serikali itaendelea na mchakato wa kutayarisha sera ya kukuza na kuendeleza sekta binafsi ambayo itawawezesha wananchi walio wengi kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa Desemba, 2003 jumla ya mashirika/makampuni na mali za mashirika 617 yalibinafsishwa ikijumuisha mashirika/makampuni 289 na mali zisizokuwa muhimu *(Non Core Assets)* 328. Katika kipindi cha mwaka 2003 ubinafishaji ulikuwa ni makampuni/mashirika 26 na mali zisizokuwa muhimu *(Non Core Assets)* 75. Mashirika haya yamebinafishwa kwa Watanzania na wawekezaji kutoka nje na mengine kwa njia ya ubia. Mengi ya mashirika hayo yanafanya kazi kwa ufanisi na kutoa gawio na kodi Serikalini, kutoa nafasi za ajira na kuwezesha upatikanaji wa manejimenti na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 kazi zilizokamilika ni ukodishaji wa mamlaka ya majisafi na majitaka *(DAWASA),* ubinafsishaji wa Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo *(SPM)* na kampuni za hoteli za *TAHI* na tafiti mbili kwa ajili ya kuligawanya Shirika la Umeme *(TANESCO)* katika kampuni tatu ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa maandalizi ya kuunda mfumo mpya wa utendaji wa soko la nishati ya umeme na mkataba wa utendaji wa menejiment kwa kipindi maalum. Kwa upande wa Shirika la Reli taratibu za ukodishaji wa muda mrefu zimefikia hatua ya kuitisha zabuni kwa wawekezaji walioonyesha nia ya kukodi Shirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2004/2005 itaendelea kukamilisha ubinafsishaji wa mashirika ya umma yaliyobaki ambayo ni pamoja na *NMB,* Vitengo vya kibiashara vya *THA* vilivyosalia, *TANESCO, TRC, TAZARA, NIC,* Viwanda vya Korosho, mashamba ya *NAFCO,* mashamba ya mifugo ya *NARCO* na kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji vya mashirika yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 4.0 ikiwa ni pungufu kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5 mwaka 2002. Upungufu huu ulitokana na pamoja na ukosefu wa mvua hususan katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Morogoro, Pwani, Arusha, Manyara na Tabora.

Mikoa mingine ambayo nayo ilikabiliwa na ukosefu huo ni pamoja na Mbeya, Iringa, Lindi, Mara, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro na Mtwara. Mchango mkubwa wa ukuaji wa mwaka 2003 ulitokana na sekta ya uvuvi asilimia 6.4, sekta ndogo ya mifugo asilimia 5, misitu na uwindaji asilimia 4.2. Sekta ndogo ya mazao ya kilimo ambayo ndiyo mara kwa mara inayochangia kwa kiwango kikubwa, ilikua kwa asilimia 3.6 mwaka 2003 ikiwa ni chini ya ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa Pato la Taifa kunategemea kwa kiasi kikubwa ukuaji katika sekta ya kilimo. Serika katika kunusuru uchumi usiathirike kutokana na ukosefu wa mvua uliotokea mwaka 2003/2004, ilichukua hatua za haraka zifuatazo:-

(i) Kutoa jumla ya shilingi 2.0 bilioni kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

(ii) Kufanya ukarabati mkubwa wa vituo 17 kati ya vituo 22 vya utafiti. Aidha, vituo vyote 22 vimepatiwa vitendea kazi muhimu. Matokeo ya juhudi hizi ni kuzalishwa

kwa mbegu mpya kwa mazao kama vile ya kunde, matunda, mkonge, migomba, viazi vitamu, muhogo n.k. Jumla ya tani 12,500 za mbegu mbalimbali zilizalishwa.

(iii) Kuongeza uwezo wa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, kukopesha pembejeo kupitia mabenki na Vyama vya Ushirika kwa mikataba. Mabenki yaliyohusika ni pamoja na Benki ya Wananchi Mufindi, Benki ya Ushirika ya Wakulima Kagera, Benki ya Exim, Benki ya Ushirika Kilimanjaro na Shirikisho la Vyama vya Kuweka na Kukopa Tanzania *(SCCULT).*

(iv) Kununua, kusafirisha na kusambaza hadi Mikoani matrekta 170. Vile vile iliendelea kutoa mikopo ya kukarabati matrekta machakavu.

(v) Kukamilisha maandalizi ya sehemu ya kwanza ya mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Uchuguzi umeonyesha kuwa Taifa lina hekta milioni 29.4 zinazofaa kuendelezwa kwa umwagiliaji maji kati ya hizo hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa. Eneo liloendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji ni hekta 200,895.

(vi) Kuwashirikisha na kuwahusisha wadau wa mazao ya Chai, Kahawa na Tumbaku katika uendeshaji na usimamizi wa utafiti wa mazao hayo kwa kuanzisha Taasisi za utafiti zilizo nje ya mfumo wa Kiserikali zinazowajibika moja kwa moja kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuiondoa jamii yetu katika tatizo la uhaba wa chakula wa mara kwa mara hatuna budi kupitia upya utekelezaji wa mikakati mbalimbali tuliyojiwekea ili kukuza kwa kasi sekta ya kilimo na mifugo. Kwa mwaka 2004/2005 Serikali itaendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kwa kujenga skimu za umwagiliaji maji, kuboresha huduma za ugani na utafiti ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo na mbegu bora. Aidha, mtandao wa barabara kuu na za vijijini utaboreshwa kwa vile unachangia katika ongezeko la ukuaji wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali kimsingi kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Jukumu la uanzishaji wa Benki hiyo linasimamiwa na Wizara ya Fedha ikishirikiana na Benki Kuu. Madhumuni ya Benki hiyo ya maendeleo ni kutoa huduma ambazo mabenki ya kibiashara na vyombo vya fedha havipo tayari kutoa kwa sekta zote muhimu za kilimo, viwanda, na kadhalika, hivyo mpango wa Serikali wa kuanzisha benki hiyo unatarajiwa kuleta nafuu kubwa katika utoaji wa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, masoko na usindikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuanzisha chombo kama hicho inahitaji uangalifu na umakini wa hali ya juu. Hivyo lazima uchunguzi wa kina ufanywe na wataalam ili kubainisha mazingira mazuri ya uendeshaji wa chombo hicho. Uchunguzi huo wa kina sharti uzingatie *profile* ya wakopaji watarajiwa na *risk factors,* zilizopo kwenye shughuli za kilimo na hata viwanda ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa wananchi. Hivyo ni vyema ieleweke kwamba muda wa kutosha unahitajika ili kufanya kazi ya uanzishaji wa chombo hicho muhimu.

Aidha, hatua ambazo zimekwishachukuliwa ni pamoja na kupokea maoni na mapendekezo ya jinsi ya kuanzisha na kuendesha Benki ya Maendeleo kutoka Benki Kuu na Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC).* Mapendekezo haya yanafanyiwa kazi na ushauri utawasilishwa Serikalini ili kuweza kuanza hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, jitihada zilizotajwa hapo juu zinawiana na zile zinazotekelezwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi ya Kusini mwa Afrika, kama ilivyobainishwa kwenye mkutano usiokuwa wa kawaida wa viongozi wa nchi za *SADC* uliofanyika Mei 15, 2004 Jijini Dar es Salaam. Aidha, masuala yafuatayo yatatekelezwa katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika kukabiliana na uhaba wa chakula nayo ni:-

(a) Kuongeza Bajeti ya sekta ya kilimo kufikia asilimia 10 ya Bajeti ya nchi wanachama na kati ya hiyo asilimia 25 ielekezwe kwenye upatikanaji wa zana na pembejeo za kilimo ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao; *(Makofi)*

(b) Kusaidia wakulima kupata masoko ya mazao ambayo yamo kwenye nchi wanachama hususan soko la ndani la kikanda na Kimataifa;

(c) Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kutokana na michango kutoka sekta binafsi, michango kutoka kwa nchi wanachama na taasisi za kimataifa; na

(d) Kuendeleza juhudi za kuzuia maambukizi mapya ya Ukimwi yanayopunguza nguvukazi muhimu kwenye sekta ya kilimo.

Aidha, maeneo mengine ambayo yatapewa kipaumbele ni kuimarisha uzuiaji wa magonjwa ya mazao na mifugo, kuimarisha hifadhi ya maji na udongo, kuendeleza matumizi ya teknolojia ya kisasa na kuimarisha shughuli za ushirika. Pia ushiriki wa sekta binafsi katika uzalishaji na usindikizaji wa mazao ya kilimo utapewa umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.0 mwaka 2002. Ukuaji huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na viwanda vya nguo vilivyobinafsishwa na ambavyo vilikuwa vimesimamisha uzalishaji, kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo ni *Kiltex - Arusha, Mwatex, Mutex, Sunguratex, Mbeyatex* na kiwanda cha kutengeneza mablanketi cha Dar es Salaam. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha kwa sera ya viwanda na biashara ndogo na za kati *(SMEs)* ambayo imeweka mazingira bora katika kukuza viwanda na biashara ndogo na za kati;

(ii) Kuongezeka kwa miradi ya viwanda kutoka miradi 103 mwaka 2002 hadi miradi 127 yenye thamani ya shilingi 239.6 bilioni mwaka 2003; na

(iii) Kuanza kwa uwekezaji kupitia *EPZ* ambapo kiwanda cha nguo cha *NIDA Textile Mills* kilichopo Dar es Salaam kimeanzishwa. Aidha, maeneo zaidi ya uwekezaji

kupitia *EPZ* yamebainishwa katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Mtwara na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekelezwa azma ya kuanzisha Benki ya Maendeleo kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa sekta ya viwanda na ushirika, Serikali imefanya utafiti ili kubaini endapo benki ya raslimali Tanzania ingeweza kubadilishwa kuwa Benki ya Maendeleo. Utafiti huo umekamilika na taarifa yake inachambuliwa na wadau husika. Aidha, katika mwaka 2004/2005 Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha na kukuza viwanda nchini kwa kutekeleza awamu ya kwanza ya mpango unaofadhiliwa na *UNIDO* ambao unatoa kipaumbele katika viwanda vya nguo na ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 sekta ya madini ilikua kwa asilimia 17.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.0 kwa mwaka 2000. Mchango wa Sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kwa mwaka 2003 uliongezeka hadi kufikia asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2002. Aidha, katika mwaka 2003 thamani ya madini yaliyouzwa nchi za nje ilikuwa dola za Kimarekani 491.9 milioni ikilinganishwa na dola 396.1 milioni mwaka 2002 takwimu hizo zinaonyesha ongezeko la asilimia 24. Ongezeko hilo linachangiwa na kuimarika kwa shughuli za uchimbaji madini kunakofanywa na makampuni makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 sekta ya madini itaendelea na utekelezaji wa mabadiliko ya kiuchumi ambayo yanatoa kipaumbele kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza uchumi. Aidha, italenga katika kufanikisha mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha shughuli za uchimbaji wa madini zinafanyika kwa usalama zaidi na kuzingatia uhifadhi na usimamizi bora wa mazingira.

(ii) Kukamilisha taratibu za kutambua migodi itakayofungwa na kutekeleza ufungaji wa migodi hiyo.

(iii) Kuanzisha shughuli za ukataji vito na ufuaji wa dhahabu hapa nchini.

(iv) Kuhamasisha wachimbaji wadogo wadogo kwa kuboresha taratibu za utoaji leseni na usajili, kuwapatia elimu kuhusu milipuko ya baruti, afya, uhifadhi wa mazingira na kuwapatia mikopo na vifaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, sekta ya uuzaji jumla, rejareja na mahoteli ikijumuisha utalii ilikua kwa asilimia 6.5, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2002. Kushuka kwa kiwango cha ukuaji hususan utalii, kulitokana na kuwepo kwa athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matukio ya kigaidi ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo watalii walioingia nchini mwaka 2003 walikuwa 576,198 sawa na ongezeko la asilimia 0.2.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Serikali, imekusudia kuendelea kuchukua hatua zaidi zenye lengo la kukuza na kuboresha shughuli na huduma za utalii ambazo ni pamoja na kuimarisha utoaji wa mafunzo, kuendelea na jitihada za utangazaji wa vivutio vya utalii nje na ndani ya nchi na kuimarisha miundombinu kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 sekta ya ujenzi ilikua kwa kiwango sawa na kile cha mwaka 2002 cha asilimia 11.0 ukuaji huu wa wastani umetokana na maendeleo ya kazi za ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za vijijini, ujenzi wa majengo ya nyumba za kuishi, majengo ya biashara na kazi za ujenzi na ukarabati wa madaraja nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka 2003 palikuwepo na mafanikio ya kuridhisha ambapo kwa upande wa barabara kuu kilometa 5,644 na madaraja 727 yalifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometa 5,057 na madaraja 320 mwaka 2002. Kwa upande wa barabara za Mikoa, kilometa 6,587 na madaraja 907 yalifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometa 4,780 na madaraja 150 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara za vijijini, jumla ya kilometa 5,680 na madaraja 80 yalifanyiwa matengenezo mwaka 2003 ikilinganishwa na kilometa 3,780 na madaraja 180 mwaka 2002. Vile vile Serikali imeendelea kuratibu masuala ya usalama barabarani, udhibiti wa uchukuzi wa mizigo kulingana na viwango vilivyowekwa na mafunzo ya makandarasi wazalendo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha barabara muhimu zinazounganisha mkoa na mkoa na za vijijini hasa zile zitakazowezesha kufufua sekta ya kilimo, utalii na kuvutia wawekezaji hususan katika sekta za viwanda na madini. Maandalizi muhimu yamekwishafanyika na kazi za ujenzi na ukarabati zimeanza kwa kutengeneza barabara kama ifuatavyo:-

Somanga - Masaninga/Matandu (kilometa 330), Nangurukuru - Lindi (kilometa 165), Lindi - Mingoyo (kilometa 25), Dodoma- Manyoni (kilometa 127) na Manyoni - Singida (kilometa 19 ). Barabara hizi zinajengwa kutumia fedha za ndani ambapo Wizara ya Fedha hutenga shilingi 1.84 bilioni kila mwezi. Lengo ni kukamilisha ujenzi wa barabara hizi ifikapo mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha barabara muhimu zinazounganisha Mkoa na Mkoa na za Vijijini hasa zile zitakazowezesha kufufua sekta ya kilimo, utalii na kuvutia wawekezaji hususan katika sekta za viwanda na madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi ilikua kwa kiwango cha asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2002. Mchango wa sekta katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.4 mwaka 2003 ikiinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa ukuaji wa sekta hii kumesababishwa na kupungua kwa njia za simu za kawaida zilizounganishwa kutokana na zoezi la

ubadilishaji wa mitambo ya simu na kupungua kwa shehena za mizigo hususan mazao ya kilimo yaliyosafirishwa kwa njia za barabara kutokana na ukame ulioathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuka kwa ukuaji wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi, vile vile yapo maeneo ya sekta hii yaliyofanya vizuri. Maeneo hayo ni simu za mikononi ambazo wateja wake waliongezeka kutoka simu 805,000 mwaka 2002 hadi simu 1,298,000 mwaka 2003. Huduma za posta nazo ziliimarika kwa kuongezeka kwa barua, fedha na jumbe zilizotumwa kwa njia za *EMS.* Katika kitengo cha makontena Bandari ya Dar es Salaam, muda wa makontena kukaa bandarini ulipungua kutoka siku 13.9 hadi siku 11.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu maendeleo ya sekta za mawasiliano na uchukuzi kwa kuhakikisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma, kuweka taratibu endelevu zinazoweka mkazo katika kujenga utamaduni wa matengenezo na ukarabati wa miundombinu na kukamilisha ubinafsishaji wa mashirika yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, nishati katika mwaka 2003, uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji ulishuka kutokana na ukame na kusababisha *TANESCO* kununua umeme wa *IPTL* na kutumia mitambo ya Ubungo inayotumia mafuta. Serikali ilitoa ruzuku kwa *TANESCO* na kuepusha mgao wa umeme ambao ungeathiri ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi ya Songosongo unategemewa kuanza mwezi Julai, 2004 na utapunguza utegemezi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji na mafuta. Serikali itaendelea kuhimiza uwekezaji katika vyanzo vingine vya kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, gesi asilia, upepo na jotoardhi.

Aidha, mkazo utaendelea kuwekwa katika kukusanya takwimu za vyanzo hivi, kuhimiza matumizi bora ya nishati na utekelezaji wa miradi ya matumizi ya majiko sanifu ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambao unachangia katika uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuharakisha uwekezaji na upatikanaji wa umeme vijijini, Serikali inaanzisha wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency)* na mfuko wa umeme Vijijini *(Rural Energy Fund)* na pia inaanda malengo/mikakati ambayo itaweka vigezo vya kusimamia maendeleo ya umeme vijijini. Taratibu za kukamilisha uanzishaji wa vyombo hivi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, huduma za jamii, uboreshaji wa sekta ya elimu unalenga kuweka mazingira bora ya elimu ili kutoa mchango ulio imara katika kupambana na upunguzaji wa umaskini katika jamii. Ili kuwaanda watoto katika mazingira ya shule, kumekuwa na ongezeko la shule za awali 2,277 mwaka 2003 kutoka shule 9,569 mwaka 2000 hadi shule 11,846 mwaka 2003 na kuwezesha wanafunzi 774,750 kuandikishwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa MMEM umeongeza idadi ya shule kutoka 12,211 mwaka 2002 hadi 12,649 mwaka 2003. Shule binafsi pia zimeongezeka kwa idadi

kutoka shule 59 mwaka 2002 hadi shule 166 mwaka 2003. Jumla ya uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule umeongezeka kutoka 5,981,338 mwaka 2002 hadi 6,562,772 mwaka 2003. Sambamba na ongezeko la wanafunzi, madarasa 1,342 yalijengwa na walimu wapya 15,921 waliajiriwa na nyumba za walimu 226 zilijengwa.

Mheshimiwa Spika, ili mpango wa MMEM uwe na uwiano na uingiaji watoto shule za sekondari, mpango wa kuboresha shule za sekondari utatekelezwa kuanzia mwaka 2004/2005. Kwa mwaka 2003 idadi ya wanafunzi waliojiunga na sekondari iliongezeka kutoka asilimia 21.7 mwaka 2002 hadi asilimia 38.7 mwaka 2003. Uwiano wa wavulana na wasichana wanaomaliza kidato cha nne ulikuwa asilimia 53.6 kwa wavulana na asilimia 46.4 kwa wasichana.

Mheshimiwa Spika, kwa wanaomaliza kidato cha sita uwiano ulikuwa wavulana 65.5 na wasichana asilimia 34.5.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi yametupa uzoefu na dhamira ya kuwa na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari utakaoongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari kutoka asilimia 22 ya waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2003 hadi asilimia 50 ya watakaomaliza elimu hiyo mwaka 2009, tena kwa kuzingatia jinsia na mtawanyiko kijiografia ndani ya nchi.

Lengo pia ni kuongeza kiwango cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili wanaopata Daraja la I - III wafikie asilimia 70 ya wanafunzi wafanyao mtihani ifikapo mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu ya juu, Serikali inaendelea na mpango wa kusaidia kugharamia elimu nchini. Chini ya mfuko wa elimu wanafunzi watalipiwa ada kama mkopo bila riba na watatakiwa kurejesha fedha hizo mara wanapohitimu na kuanza kazi. Aidha, mpango utaboresha mazingira ya kutoa elimu katika ngazi zote kwa walimu kwa kujenga na kukarabati nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Serikali iliendelea kuimarisha mpango wa kueneza huduma ya maji kwa wananchi hususan kwa kuhimiza ushiriki wa jamii katika kuandaa, kuendesha na kutunza miradi ya maji kupitia kamati za maji. Kufikia Desemba, 2003, Bodi 30 za kusimamia mamlaka za maji zilikuwa zimeanzishwa katika Wilaya mbalimbali nchini. Vile vile kamati za maji 8,363 zilikuwa zimeanzishwa na jumla ya mifuko ya maji 7,226 ilianzishwa yenye jumla ya shilingi bilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, huduma za maji mijini pia zimeendelea kupanuka chini ya mamlaka za maji mijini. Wateja wapya wameongezeka kutoka 127,404 Juni, 2002 hadi 137,595 Juni, 2003 na ufungaji wa dira za maji umeongezeka kutoka 64,105 Juni, 2002 hadi 84,424 Juni, 2003, likiwa ni ongezeko la asilimia 24. Uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka mita za ujazo 276,000 kwa siku Juni, 2002, hadi mita za ujazo 279,116 kwa siku Juni, 2003. Pia mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 11.7 mwaka 2001/2002 hadi shilingi bilioni 13.4 mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya katika mwaka 2003, Serikali ikishirikiana na wadau wengine imeendelea kutekeleza mfumo mpya wa uendelezaji wa sekta ya afya. Mafanikio ya utekelezaji wake yameanza kuonekana katika huduma za afya zitolewazo nchini na ukarabati wa taasisi za afya ikiwemo, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali za Wilaya baadhi ya vituo vya afya. Vile vile, kumekuwepo na ongezeko la upatikanaji wa dawa katika ngazi zote na ongezeko la chanjo za kifua kikuu, polio, kifaduro, pepopunda na surua. Pamoja na hayo, jitihada za kupambana na ugonjwa wa malaria ziliendelea. Kwa msaada wa wahisani mbalimbali Serikali imeamua kutoa bure dawa za kurefusha maisha kwa waishio na Virusi vya Ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, mifuko wa afya ya jamii ilianzishwa katika Halmashauri 23 na Wilaya nyingine 17 zinakamilisha taratibu ili nazo zianze utekelezaji. Aidha, kwa wafanyakazi wa sekta ya umma, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uko katika mwaka wake wa tatu wa utekelezaji. Matatizo mengi ya awali kutokana na uchanga wa mfuko kama kukosekana kwa dawa na kutokuwepo vituo vya kutosha vya kutolea matibabu, yameanza kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 mkazo katika sekta ya afya utaendelea kuwekwa katika kufanya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya, kutoa mafunzo ya kinga juu ya magonjwa, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya mama na mtoto, kuimarisha maendeleo ya raslimali watu wa sekta ya afya na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kutendea kazi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, masuala mengineyo ya kitaifa, mkakati wa kupunguza umaskini. Huu ni mwaka wa tatu wa utekelezaji wa mkakati wa kupunguza umaskini uliotayarishwa katika kipindi cha mwaka 2000/2001. Taarifa ya tatu ya utekelezaji wa mkakati huu inabaini kuboreka na kuimarika kwa huduma mbalimbali katika sekta zinazopewa kipaumbele na Serikali katika mgao wa raslimali hususan katika elimu, afya, barabara vijijini na maji. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la asilimia 50 katika uandikishaji watoto elimu ya msingi, waliongezeka kutoka milioni 4.4 mwaka 2000 hadi milioni 6.6 mwaka 2003. Uamuzi wa Serikali wa kuondoa karo na michango mbalimbali katika shule za msingi umechangia kwa kiwango kikubwa katika ongezeko hilo.

Hata hivyo ubora wa elimu na kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari bado haujawa wa kuridhisha. Katika sekta ya afya chanjo kwa watoto wadogo *(DPT)* na chanjo dhidi ya surua zimekuwa zinaongezeka mwaka hadi mwaka hadi kufikia kiwango cha asilimia 90. Aidha, idadi ya watu wanaopata maji safi vijijini na mijini imeongezeka katika mwaka 2003 inakadiriwa kufikia asilimia 53.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.5 ikilinganishwa na mwaka 2001. Huduma ya maji mijini iliendelea kuwa asilimia 73 ikilinganishwa na asilimia 70 ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji mdogo na tija ndogo katika sekta ya kilimo, ukosefu wa ajira mijini na vijijini na kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi ni changamoto kubwa katika kuongeza kipato kwa wananchi walio wengi. Katika mwaka 2004/2005 juhudi thabiti zaidi zitafanywa ili kukuza kilimo na usindikaji wa bidhaa kwa

kuwawezesha wakulima wakubwa na wadogo, wazalishaji na wajasirimali wa kati na wadogo kupitia mifumo inayofaa ya mikopo na dhamana na taratibu za kibiashara.

Kuhusu mkakati wa Hernando De Soto wa kupunguza umaskini, katika mwaka 2003, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwalika Mshauri wa Uchumi Bwana Hernando De Soto ili kubadilishana uzoefu juu ya kuiwezesha sekta isiyo rasmi kuingia katika mfumo wa sekta rasmi. Mnamo tarehe 29 Machi, 2004, Mheshimiwa Rais aliitisha kikao kujadili taarifa ya wataalam wa uchumi kuhusu mkakati wa kubadilisha raslimali mfu kuwa hai *(Transform dead capital into live capital - Hernando De Soto Initiative).*

Mheshimiwa Rais aliagiza kila Wizara iliyohusika iandae mkakati wa utekelezaji. Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imeandaa programu ijulikanayo kama *Creation of a comprehensive Urban Land Property Register for Economic Empowerment of Residents in Unplanned Settlements in Dar es Salaam.* Programu hii itachangia sana harakati za Serikali kuwawezesha wananchi kuingia katika sekta rasmi.

Mheshimiwa Spika, lengo la mkakati huu ni kupunguza umaskini kwa kuwawezesha wananchi kuwa na umilikaji halali wa ardhi katika makazi yasiyopangiliwa kwa kuandaa leseni za makazi ambazo zitatumika kama dhamana katika taasisi za fedha kwa ajili ya kupatiwa mikopo. Mkakati huu utasimamiwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zote tatu ambazo ni Ilala, Temeke na Kinondoni. Idadi ya mali zipatazo 400,000 zitaorodheshwa kwa awamu mbili katika kipindi cha miaka miwili (2004 - 2006). Aidha, mkakati huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 3.2.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005 Serikali itaendelea na juhudi zake za kusaidia Mikoa na Wilaya kukusanya na kuweka takwimu za sekta ambazo zitawezesha upimaji wa maendeleo katika sekta mbalimbali. Aidha, Mikoa na Wilaya inahimizwa kukamilisha utayarishaji wa mipango yao ya maendeleo ya muda wa kati itakayotungamanisha malengo ya kupunguza umaskini katika kipindi cha muda wa kati.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa. Katika mwaka 2001/2002 Serikali iliweza kufungua ofisi ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa *(PCB)* katika Wilaya zote nchini na katika mwaka 2003/2004 Serikali ikishirikiana na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Kimataifa *(UNDP)* na wafadhili wengine iliendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma hapa nchini na nje ya nchi kuhusu mikakati na uzoefu wa nchi nyingine katika kuzuia rushwa na jinsi ya kutungamanisha masuala ya uzuiaji rushwa katika mipango ya Kitaifa ya Maendeleo na mfumo wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005 Serikali itaendelea kusisitiza juu ya kuziba mianya ya rushwa kwa kuweka taratibu za kisheria na utawala zitakazoweza kutoa mwelekeo sahihi na kujenga mshikamano kati ya Serikali, sekta binafsi na asasi za raia ambazo ni pamoja na mashirika yasiyo ya Kiserikali, vyombo vya habari na Mashirika au Jumuiya za kidini katika kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ushirikiano wa karibu na Jumuiya za raia na sekta binafsi, Serikali itaendelea kutekeleza malengo yaliyopo katika mkakati wa kuondoa rushwa ambao utaelekeza katika:-

- Kuinua utawala bora na kukuza maadili kati ya watumishi wa Serikali, sekta binafsi na jumuiya za kiraia;

- Kuimarisha vyombo vya usimamizi wa sheria kama vile Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Polisi na Sekretariati ya maadili na mahakama; na ya mwisho

- Kukuza ushirikiano kati ya nguzo kuu tatu za kupambana na rushwa yaani Serikali, jumuiya za kijamii na sekta binafsi katika mshikamano kwa ajili ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2003, Tanzania ilikadiriwa kuwa na nguvu kazi inayozidi watu milioni 17.8 kati ya hao asilimia 75 wanaishi maeneo ya vijijini. Pia ilikadiriwa kuwa, karibu watu 700,000 wanajiunga na soko la ajira kila mwaka.

Aidha, watu wasio na kazi kwa nchi nzima, kufikia kipindi hicho cha Desemba, 2003 wanakadiriwa kuwa asilimia 12.9 Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na asilimia 46.5 miji mingine asilimia 25.5 na vijijini asilimia 8.4. Ongezeko la watu wasio na ajira mijini limetokana na hali mbaya ya uchumi katika maeneo ya vijijini na hivyo kufanya vijana kuhamia maeneo ya mijini kwa tegemeo la kupata ajira, ambako pia ni chache. Uboreshaji wa miundombinu na huduma vijijini utachangia kupunguza kasi ya sehemu ya nguvu kazi kukimbilia mijini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana mwaka 2003 katika kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira ni kuhuisha sera ya Taifa ya ajira, ambayo ipo katika hatua ya mwisho kupitishwa na Serikali. Sera hii itajenga mazingira yanayowezesha sekta binafsi, mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na vikundi vya jamii *(CBOs)* kushiriki kikamilifu katika ukuzaji wa ajira.

Aidha, katika kuwahimiza wananchi wajiajiri wenyewe, Serikali katika mwaka 2003 iliendelea kuhamasisha maendeleo ya vikundi vya kuweka na kukopa *(SACCOS),* ambazo kumekuwepo na ongezeko kutoka vikundi 927 mwaka 2002 hadi kufikia vikundi 1,264 Desemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Serikali inatarajia kuanzisha mpango wa kubainisha na kutambua kisheria mitaji na raslimali za watu waliojiajiri katika sekta isiyo rasmi, kubaini na kuondoa vikwazo vinavyofanya iwe vigumu kwao kuingia kwenye sekta rasmi inayotambuliwa kisheria. Aidha, Bajeti ya Serikali itatumika katika kuchochea upatikanaji wa ajira kwa kutumia sera za mapato na matumizi, hasa kupitia mifuko ya udhamini na mikopo kwa wawekezaji wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, jinsia, uchambuzi wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 umebainisha kuwa asilimia 33 ya kaya nchini zina wakuu wa kaya wanawake. Hii ni jumla ya kaya takribani 2,311,000. Katika uchambuzi huo kiumri imebainika pia kuwa wapo watoto walio chini ya umri wa miaka 18 ambao ni wakuu wa kaya zipatazo 74,000. Kati ya kaya hizo asilimia 45 ya wakuu wa kaya hao ni watoto wa kike. Uchambuzi unaendelea ili kubainisha mahusiano haya katika maeneo mengine ya takwimu za sensa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003 Serikali kwa kushirikiana na taasisi zisizo za Kiserikali iliendeleza juhudi zake za kuingiza masuala ya kijinsia katika sera, mipango na maendeleo ya ugawaji wa raslimali *(resource allocations).* Vile vile kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania *(TGNP)* kulitolewa miongozo na mafunzo katika Wizara mbalimbali juu ya kuingiza vionjo vya kijinsia katika sera, mipango ya maendeleo na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kijacho Serikali itaendelea kuboresha ukusanyaji wa takwimu ili ziweze kubainisha masuala ya kijinsia na kutengeneza viashiria bainishi na kuviingiza katika mpango kamambe wa ufuatiliaji wa umaskini *(Poverty Monitoring Master Plan).* Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya jinsia, Serikali itatekeleza mikakati iliyojiwekea katika mpango wake wa muda wa kati kwa kipindi cha 2004/2005 - 2006/2007, ambayo ni pamoja na:-

- Kuendelea kutoa elimu ya jinsia katika ngazi zote.

- Kuendelea kuziimarisha na kuziwezesha taasisi husika.

- Kuongeza Bajeti katika shughuli za kuingiza masuala ya jinsi kwa ajili ya kuweza kutengeneza mfumo wa ufuatiliaji wa tathmini ya umaskini katika ngazi zote.

- Uhamasishaji utakaopelekea kuwepo na mikakati ya kumaliza tatizo la kukosekana usawa wa kijinsia.

- Kutengeneza na kutumia takwimu zinazohusisha mahusiano ya kijinsia katika sera zetu na kuongeza ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika masuala ya umilikaji wa mali na fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Taifa wa kudhibiti Ukimwi, bado idadi ya wananchi walioambukizwa inaendelea kuongezeka na kufikia karibu milioni 2.2 mwaka 2003. Wengi wa walioambukizwa ni wale ambao wako katika umri kati ya miaka 20 na 49 wengi wao wakiwa katika umri kati ya miaka 25 - 34 kwa wanawake na miaka 30 - 39 kwa wanaume. Kundi hili ndilo kundi ambalo ni la nguvukazi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kuathirika kwa kundi hili kutaleta madhara makubwa katika kukua kwa uchumi na ustawi wa jamii. Vijana wengi nchini walio chini ya miaka 20 nao ama wameambukizwa Ukimwi kama hawatachukua hatua ya kujikinga. Ni jukumu la

viongozi wote wa Serikali, sekta binafsi, taasisi za dini, *NGOs, CBOs* vyama vya siasa na kadhalika, kuendelea kuelezea athari za Ukimwi na kuhimiza kujiepusha na janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba zinachukuliwa hatua za kupambana na tatizo la kuenea kwa ugonjwa huu katika ngazi za chini, Serikali za mitaa zitasaidiwa katika kuandaa mipango mahsusi itakayowashirikisha wadau wote. Taasisi za Mikoa za kutoa ushauri zitatoa misaada ya kitaalam kwa Serikali za mitaa na mashirika ya kijamii ili kuzipa uwezo jamii za vijijini na mijini ili nazo ziweze kuweka mikakati mizuri ya kuweza kuzuia kuenea kwa Ukimwi katika maeneo yao. Mfumo wa kuratibu na kupima maendeleo yatakayofikiwa kuhusu kupunguza kuenea kwa Ukimwi umeshaandaliwa na wakufunzi maalum pia wameshaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 1999 Serikali ilipitisha na kuridhia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Dira ya maendeleo ndiyo nguzo kuu ya kuunganisha nguvu zetu kama Taifa katika kupambana na umaskini na kujenga uchumi imara na endelevu na kuondokana na matatizo sugu ambayo nimeyaelezea katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2000, Serikali katika ngazi ya Taifa imejitahidi kuweka misingi imara ya kutekeleza malengo mapana ya Dira kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutunga na kuhuisha sera za uchumi jumla na sera za kifedha zinazolenga katika kutengemaza vigezo vya uchumi jumla, ili kujenga uchumi unaokua na wenye ushindani;

(ii) Kutunga na kurekebisha sheria na kanuni za kuongoza taratibu za uwekezaji raslimali nchini na kusimamia soko huria;

(iii) Kuwezesha kila sekta kuwa na sera, mkakati na malengo ya kisekta yanayoendana na malengo muda wa kati ya Dira 2025;

(iv) Kuanzisha vyombo vya kuratibu na kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali kujenga miundombinu na kutoa huduma za kijamii; na

(v) Kutayarisha na kutekeleza mkakati wa kuondoa umaskini, mkakati wa kuondoa umaskini, mkakati wa kukuza sekta ya kilimo na mkakati wa kuleta maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho pia Serikali ilibuni Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Wanawake, Sera ya Mikopo Midogo *(Microfinance)* Mpango wa Kuboresha Sekta ya Elimu, Mkakati wa Utengenezaji wa Barabara, Mkakati wa Taifa wa kuzia Maambukizi ya Ukimwi na Sera ya Uanzishaji wa viwanda vidogo na vya kati. Mikakati na Sera hizo zina lengo la kurahisisha na kuharakisha utekelezaji wa Dira 2025.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujenga mazingira sahihi yanayorahisisha utekelezaji wa malengo yaliyopewa kipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ni muda muafaka kwa Mikoa na Wilaya kukamilisha utayarishaji wa Mipango ya Maendeleo ya muda wa kati kama vyombo vya kutekeleza Dira katika maeneo husika. Utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa muda wa kati unaowiana kisekta na unaoshirikisha wadau wote katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ni changamoto itakayohakikisha kuwa mafanikio tunayoyapata katika kutekeleza sera za uchumi jumla yanatiririka na kuwanufaisha wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa vitabu vya Mpango wa Muda wa Kati 2004/2005-2006/2007 vinavyobainisha sera, mikakati na malengo ya sekta zote vilivyotayarishwa ili kukidhi shabaha ya kuongoza Wizara, Mikoa na Wilaya katika zoezi zima la kutayarisha mipango ya muda wa kati 2004/2005-2006/2007.

Aidha kwa mwaka 2004/2005 Mpango wa muda wa kati uliowasilishwa utaboreshwa zaidi kwa nia ya kutungamanisha na mkakati wa kupunguza umaskini ili hatimaye Taifa liongozwe na mpango mmoja wenye sera, mikakati na malengo yanayoeleweka kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, misingi, matarajio na malengo ya mpango na Bajeti kwa mwaka 2004/2005, misingi na matarajio yaliyozingatiwa katika kuandaa mpango wa muda wa kati na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 ni pamoja na matumaini kwamba hali ya hewa itakuwa nzuri, utulivu na amani vitaendelea kuwepo nchini na duniani, fikra za maendeleo na kujituma zitakomaa katika jamii, Serikali itaendelea kuboresha sera zake za kiuchumi na kifedha zinazolenga katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini na sekta binafsi itaendelea kukuzwa ili iweze kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika Pato la Taifa. Kwa kuzingatia misingi na matarajio hayo malengo ya sera za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2004/2005 - 2006/2007 yanatarajiwa kuwa kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa halisi linakadiriwa kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2004, asilimia 6.5 mwaka 2005, asilimia 6.9 mwaka 2006 na asilimia 7.4 mwaka 2007;

(ii) Kasi ya upandaji bei itapungua hadi kufikia asilimia 4.0 ifikapo Juni, 2005 na baadaye kupungua kwa kulingana na viwango vitakavyokuwepo katika nchi tunazofanya nazo biashara;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa, kwa bei za miaka husika, kwa asilimia 15.9 mwaka 2004/2005 hadi asilimia 16.2 ifikapo mwaka 2006/2007;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana) litakalowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi sita.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo mpango umeainisha vipaumbele vya kupewa msukumo maalum katika miaka mitatu ya kwanza ikiwa ni tafsiri ya kiutekelezaji wa malengo mapana na ya muda mrefu na ya kati yaliyowekwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2005. Vipaumbele hivyo ni:-

(i) Uendelezaji raslimali watu, ikiwa ni pamoja na kuendeleza elimu na ujuzi, afya na kujiamini kwa wananchi;

(ii) Kujenga uhakika na usalama wa chakula ili kukidhi mahitaji ya wananchi ya lishe na hatimaye kusukuma harakati mbalimbali za maendeleo bila kuyumbishwa na uhaba wa chakula;

(iii) Kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kuchochea ongezeko la uzalishaji kwa kuipatia nchi uwezo wa kununua kutoka nje malighafi na teknolojia; na

(iv) Kukuza ajira ili kukabiliana na ukosefu wa ajira nchini ambao ni tatizo linalozidi kukua na kusababisha idadi ya watu walio katika hali ya umaskini kuzidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, majumuisho, kabla sijamaliza hotuba yangu napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza masuala ambayo Taifa linapaswa kuyapa kipaumbele na Wizara husika zikishirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kufuatilia.

Kwanza, kuhakikisha kuwa Sera na mikakati mbalimbali inayotekelezwa hivi sasa na inayolenga katika kukuza sekta ya kilimo ni thabiti, endelevu na inaleta unafuu wa kudumu katika kuwapatia wananchi chakula na kuinua vipato vyao.

Pili, kuimarisha na kusaidia sekta isiyo rasmi ili ipate kupanuka na kutengemaa kwa lengo la kuongeza nafasi za ajira nchini. Katika ngazi zote sekta isiyo rasmi ipewe furasa na haki ya kumiliki raslimali na mitaji, ikiwemo nguvu zao na ardhi kama mbinu ya kuwawezesha kuingia katika mfumo rasmi wa uchumi. Juhudi muhimu hapa ni kuzibaini, kuzisajili na pengine kuzipima kwa mfano ardhi, raslimali katika sekta isiyo rasmi.

Tatu, kusimamia uundaji wa mabenki/taasisi za kifedha zitakazorahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta muhimu za kilimo na viwanda na nne, kuhimiza wawekezaji wa ndani kuwekeza raslimali zao katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mazao ya wakulima ili kuongeza thamani ya mauzo nje na kupanua nafasi za ajira nchini.

Tano, kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba ambayo itawezesha wananchi kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kuzalisha mali na kutoa huduma. Suala la uhamasishaji wa wananchi kujiwekea akiba ni la msingi na sita kuweka mfumo ambao utahakikisha kwamba shughuli zetu zote za maendeleo katika ngazi zote za utendaji, Taifa, Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinazoongozwa na Dira, Sera, Mikakati na malengo yanayoeleweka na kutekelezeka. Aidha, katika kuandaa na kutekeleza Mipango yetu ya

maendeleo ya muda wa kati katika ngazi zote, hatuna budi kujiwekea utaratibu mzuri na uliowazi wa kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, saba ni kujizatiti na kuchukua hatua za makusudi kupunguza kiwango chetu cha kutegemea misaada kutoka nje hususan katika Bajeti ya Serikali iwe ni wajibu wa kila mmoja wetu kuona ni kwa namna gani tunaweza kuchangia katika kukuza uchumi na kuhamasisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika maeneo yetu na

Mwisho, kubainisha na kutayarisha mfumo thabiti wa ufuatiliaji utakaokidhi ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na mikakati ya maendeleo kufuatana na malengo ya Dira ya Maendeleo 2025 na Mkakati wa Kupunguza Umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba njia pekee ya kuinua kiwango cha kukua kwa uchumi wetu ni kuongeza tija, juhudi na ubunifu katika ngazi zote za utendaji na utekelezaji katika sekta binafsi na sekta ya umma. Serikali itafanya yale yaliyo ndani ya dhamana na uwezo wake hasa katika kuweka mazingira bora, lakini tegemeo kuu la kuweza kubadilisha hali yetu ni wananchi kushiriki katika fursa zilizopo na kuongeza tija kwa kasi kubwa zaidi. Hivyo, kila Kijiji, Kata, Tarafa na kila Wilaya hadi ngazi za Mkoa, walenge kubainisha yale wanayoweza kuyafanya kwa kutumia fursa na raslimali zilizoko katika maeneo yao. Serikali Kuu itabakia na changamoto ya kuunga mkono juhudi hizo za dhati kulingana na uwezo wake. Kwa njia hii, nina hakika kasi ya maendeleo yetu itapanda mwaka hadi mwaka hadi kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, sera na msimamo wa Serikali ni kudumisha ushirikiano mzuri wa kidiplomasia uliopo kati yetu na nchi karibu zote duniani pamoja na taasisi za Kimataifa na Mashirika mbalimbali kwa manufaa yetu sote. Kwa hiyo, tutakuwa tumekosa fadhila tusipotambua misaada na michango ya baadhi ya nchi, taasisi za Kimataifa na Mashirika mbalimbali walioshirikiana nasi katika harakati za kuinua uchumi wetu na katika mapambano ya kuondoa umaskini. Naomba sasa nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliotusaidia na kutoa pongezi zetu za dhati kwa kuzitaja, nchi, taasisi na mashirika kama ifuatavyo:-

Serikali za Uswisi, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Afrika ya Kusini, Japan, Kuwait, Italia, Ireland na nchi nyingine marafiki.

Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* Mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD* na *WHO,* Jumuiya ya nchi za Ulaya *(EU)* na mfuko wa fedha wa nchi wanachama wa uzalishaji mafuta *(OPEC Fund).*

Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD),* Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Maendeleo la Finland *(FINNIDA),* Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na mashirika mbalimbali ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali *(NGOs). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na kama ilivyo kawaida yetu itajadiliwa pamoja na Hotuba ya Bajeti itakayotolewa baadaye mchana leo. Hadi sasa waliokwisha kujiandikisha kuchangia hoja hizi mbili ni Waheshimiwa Wabunge 45. Lakini orodha bado iko wazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya maelezo hayo sasa nitasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni, siyo 11.00 jioni kama kawaida, hadi saa 10.00 leo jioni tutakapomsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitoa Hotuba ya Bajeti. Shughuli zinasitishwa hadi saa 10.00 jioni.

*(Saa 05.34 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza, ninapenda kuwafahamisha kwamba Wageni wa Kimataifa walioko katika *Gallery* ni Waheshimiwa Mabalozi wa nchi za nje wapatao 12 ambao wote tunawakaribisha. *(Makofi)*

Kwa upande wa Watanzania ni pamoja na Makamu wa Rais wa Kwanza na Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanganyika, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Takwimu zinazoelezea kwa undani Bajeti hii ziko kwenye vitabu vinne ambavyo ni sehemu ya Bajeti hii. Kitabu cha kwanza kinahusu Makisio ya Mapato, Kitabu cha pili na cha tatu vinahusu Makisio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara, Mikoa pamoja na Halmashauri za Miji na Wilaya. Kitabu cha nne kinaelezea Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti, hususan Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge na Kamati za Kisekta; kwa kazi zao nzuri za kuchambua makisio yote kwa kina. Ushauri uliotolewa na Kamati hizo umesaidia sana kuboresha Bajeti ninayowasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Bajeti hii yamehusisha wadau wengi ndani na nje ya Serikali. Napenda kuwashukuru wote waliochangia ambao ni pamoja na wafanyakazi wa Wizara mbalimbali, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri zote za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, Asasi zisizo za Kiserikali pamoja na sekta binafsi, kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha utayarishaji wa Bajeti hii.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha Miswada na Nyaraka mbalimbali za Sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Nawashukuru pia wenzangu wa Wizara ya Fedha, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Makatibu Wakuu Bwana Gray S. Mgonja na Bwana Peniel M. Lyimo, Manaibu Katibu Mkuu, Bwana Ramadhani Khijjah na Bwana Wilfred Nyachia, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wengine wote, kwa michango yao iliyowezesha Bajeti hii kukamilika. Vile vile, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha kwa wakati hotuba hii, vitabu vya Bajeti pamoja na nyaraka nyingine zinazohusu Bajeti hii.

Mwisho, nawashukuru wale wote waliowasilisha kwangu mapendekezo yao ya kodi mpya au ya kurekebisha kodi zilizopo na pia wataalam wote waliotoa ushauri kuhusu sera na namna ya kutoza kodi mbalimbali nchini, pamoja na matumizi ya mapato yetu ambapo mengi yamezingatiwa katika kuandaa Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha tumeshuhudia kuundwa rasmi kwa Bunge la Afrika. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika Bunge hilo ambao ni Mheshimiwa Gertrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W.A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani Zanzibar na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe. *(Makofi)*

Aidha, pongezi za pekee nazitoa kwa Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge hilo. Uchaguzi wake unaonyesha imani kubwa waliyonayo Wabunge wa Bunge la Afrika kwake binafsi na kwa Tanzania kwa ujumla. Sina shaka kwamba Mheshimiwa Mongella ataifanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa ili kufanikisha malengo ya Bunge hilo na hivyo kuiletea heshima nchi yetu. *(Makofi)*

Napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuteuliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Naamini kwamba uteuzi huo si wa kubahatisha bali unaonyesha imani waliyo nayo Wajumbe wa Baraza hilo kwa Mheshimiwa Ntagazwa na kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge Viti Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa *SADC* yaani *SADC Parliamentary Forum.* Narudia tena kuwapongeza wote na ninawatakia kazi njema katika majukumu hayo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka kwamba, tarehe 30 Mei, 2004 kulifanyika uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Bariadi Mashariki, Mkoa wa Shinyanga, ambao umemrudisha Bungeni Mheshimiwa Danhi Makanga... *(Makofi/Vigelegele)*

Umemrudisha Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kishindo na kwa tiketi ya CCM. Uchaguzi huo ulifuatia mtafaruku baina yake na Chama chake cha UDP ambapo ilibidi akihame Chama hicho na kurejea tena kwenye Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Nampongeza Mheshimiwa Makanga kwa ushindi wake katika uchaguzi huo na pia wananchi wa Bariadi Mashariki kwa kutorudia kosa la kutokiri umaarufu wa CCM na kukubalika kwa Mheshimiwa Makanga miongoni mwa wapiga kura wa Bariadi Mashariki. *(Makofi/Vigelegele)*

Aidha, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba katika mwaka huu wa fedha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alimteua Mheshimiwa Makongoro Nyerere kuwa Mbunge. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Makongoro Nyerere kwa uteuzi huo na kwa kurejea kwenye Chama alicho asisi hayati baba yake ambaye ni Baba wa CCM na wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio mengine muhimu yaliyotokea mwaka huu wa fedha ni pamoja na kuteuliwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na pia Mtanzania mwenzetu, Profesa Anna Tibaijuka, kuwa Makamishna katika Kamisheni ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair. *(Makofi)*

Kamisheni hii ina jukumu la kutathmini vikwazo ambavyo vimekuwa vikirudisha nyuma maendeleo ya Bara la Afrika na kupendekeza nini kifanywe kuondokana navyo. Uteuzi wa Rais Mkapa umetokana na juhudi zake za kuyapa kipaumbele matatizo ya Bara la Afrika, hususan matatizo ya maendeleo na umaskini uliokithiri pamoja na ufahamu wa Rais Mkapa wa masuala ya utandawazi. Uzoefu wake kama Rais wa nchi ya Kiafrika inayojizatiti kupiga vita umaskini na kuleta maendeleo ya wananchi wake unatambulika duniani. Sote tunajivunia uteuzi huo wa Rais Mkapa na wa Profesa Anna Tibaijuka ambaye ni Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Makazi duniani. Tunawapongeza Watanzania hao kwa kazi nzito wanazoufanyia ulimwengu na heshima kubwa wanayoiletea nchi yetu katika kutekeleza majukumu hayo mazito mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali ya uchumi katika mwaka 2003/2004 inaonyesha maendeleo ya kuridhisha, licha ya ukame ulioikumba nchi yetu. Takwimu za awali zinaonyesha kwamba uchumi ulikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2003 badala ya lengo letu la asilimia 6.3. Kasi ya mfumuko wa bei iliongezeka kidogo kutoka asilimia 4.0 mwezi Julai, 2003 hadi asilimia 4.6 mwezi Machi, 2004. Mfumuko wa bei ulitokana na upungufu wa chakula kutokana na ukame pamoja na ongezeko kubwa la bei ya mafuta ya petroli. Akiba ya fedha za kigeni mwishoni mwa Machi, 2004 ilifikia uwezo wa

kugharamia mahitaji muhimu kutoka nje kwa kipindi cha zaidi ya miezi nane ambayo ni zaidi ya lengo la miezi sita.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004, umekuwa wa kuridhisha licha ya dharura iliyoletwa na ukame hasa katika kuongeza mahitaji ya fedha ya Bajeti kwa ajili ya kununua na kusambaza chakula pamoja na kulazimika kutoa ruzuku kwa *TANESCO* kwa ajili ya kununulia mafuta ya kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme na kununua umeme wa mtambo wa *IPTL*.

Katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, Serikali ililenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua asilimia 13.3 ya Pato la Taifa. Ili kufanikisha lengo hili, Serikali ilikusudia kutekeleza hatua kadhaa za kurekebisha mfumo na utawala wa kodi. Marekebisho hayo yalilenga kupanua wigo wa kodi, kuongeza uwajibikaji kwa watoza kodi na walipa kodi, kuondoa kodi za kero, kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuongeza ufanisi wa utendaji katika Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, Sheria mpya ya Kodi ya Mapato iliwasilishwa na kupitishwa Bungeni mwezi Aprili mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya mwaka huu wa fedha yaani kuanzia Julai, 2003 hadi Aprili, 2004 ukusanyaji wa mapato ya ndani umevuka lengo kwa kila mwezi. *(Makofi)*

Aidha, misaada ya Bajeti kutoka kwa nchi wafadhili, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Umoja wa Ulaya, ilivuka lengo. Sehemu kubwa ya misaada hiyo ilipatikana katika nusu ya kwanza ya mwaka huu wa fedha na hivyo kutupa uwezo zaidi wa kumiliki Bajeti hiyo. Inatarajiwa kwamba malengo ya mapato ya ndani na misaada ya Bajeti kwa mwaka huu yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mapato halisi ya ndani kwa kipindi cha Julai, 2003 hadi Machi, 2004 yalifikia shilingi trilioni moja, bilioni themanini na tisa, milioni mia mbili sitini na mbili (1,089,262 milioni) sawa na asilimia 3.7 au shilingi milioni 38,396 zaidi ya makisio ya Bajeti ya shilingi trilioni moja, bilioni hamsini, mia nane sitini na sita milioni (1,050,866 milioni). Kodi ya *VAT* kwenye mauzo ya ndani ya nchi ilikadiriwa kuwa shilingi milioni 142,242 katika kipindi hicho lakini makusanyo halisi yalifikia shilingi milioni 148,632 ambayo ni ziada ya shilingi milioni 6,390 au asilimia 4.5 juu ya makisio kwa kipindi hicho.

Kwa upande wa Kodi ya Mapato, makusanyo halisi yalifikia shilingi milioni 256,888 ikilinganishwa na makisio ya shilingi 227,382 milioni, sawa na ziada ya shilingi milioni 29,506 au asilimia 13 juu ya makadirio. Ukusanyaji wa Ushuru wa Forodha ulifikia shilingi milioni 95,239 ukilinganishwa na makadirio ya shilingi milioni 93,562, na hivyo kuwa na ziada ya shilingi milioni 1,677 sawa na asilimia 1.8 juu ya makadirio. Aidha, mapato yasiyo ya kodi *(non-tax revenue)* yakijumuisha mapato ya Wizara, Idara mbali mbali na Mikoa, yalifikia shilingi milioni 87,368 ikiwa ni chini ya lengo la shilingi milioni 96,951.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu zilizochangia kuongezeka kwa Mapato ya Serikali ni pamoja na usimamizi na utawala bora wa ukusanyaji wa kodi hasa Kodi ya

Mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT).* La muhimu zaidi ni zile hatua tulizochukua kudhibiti ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ya petroli. Kwa muhtasari matokeo mazuri ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni pamoja na haya yafuatayo:-

(1) Marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Forodha ambayo yameipatia Serikali mapato ya shilingi milioni 1,717 kwa kipindi cha Julai, 2003 hadi Machi, 2004 ikilinganishwa na lengo la shilingi milioni 133.8 kwa mwaka 2003/2004. Hii ni sawa na ziada ya asilimia 1,183. *(Makofi)*

(2) Marekebisho ya Ushuru wa bidhaa katika bidhaa mbalimbali yaliyoipatia Serikali mapato ya ziada ya shilingi milioni 758.5 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2003.

(3) Kupunguzwa kwa ushuru wa bidhaa kwa gesi ya kupikia *(LPG)* kutoka shilingi 228 hadi shilingi 114 kwa kilo, kulikoongeza uagizaji wa gesi hiyo kwa asilimia 52.6 kama ilivyotarajiwa.

(4) Msamaha wa kodi uliotolewa kwa mitambo ya kuchimbia visima vya maji ambao umeonyesha matokeo mazuri. Mitambo ya aina hii iliyoagizwa imeongezeka kwa asilimia 68 kutoka shilingi milioni 12,602.1 mwaka 2002 hadi shilingi milioni 21,187.8 mwaka 2003. *(Makofi)*

(5) Nafurahi kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba hatua zilizochukuliwa kudhibiti ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ya petroli zimezaa matunda yaliyotarajiwa. Jumla ya shilingi milioni 226,036 zimekusanywa kwa kipindi cha Julai, 2003 hadi Aprili, 2004, kulinganisha na lengo la shilingi milioni 208,002. Kiasi hiki ni asilimia 25 zaidi ya Kodi za Mafuta zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. *(Makofi)*

(6) Nasikitika kwamba Kodi ya Mauzo ya nje ya asilimia 15 kwa ngozi ghafi iliyoanzishwa mwaka huu wa fedha ili kuvutia usindikaji wa bidhaa hiyo hapa nchini, haijawa na matokeo yaliyokusudiwa kwani mapato yaliyopatikana katika nusu mwaka ya kwanza ni shilingi milioni 413 kulinganisha na lengo la shilingi milioni 1,080 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2003. Eneo hili litachunguzwa zaidi mwaka huu kwa lengo la kuwezesha kusindika ngozi zote hapa nchini kwa manufaa ya wafugaji na uchumi wa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo kamili ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kuongeza mapato yatafahamika baada ya mwisho wa mwezi huu, lakini mifano michache niliyoielezea ni ushahidi tosha kwamba sera nzuri, utawala bora na usimamizi imara katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, huongeza mapato. Serikali itaendelea kusimamia mambo haya na mengine mapya ambayo nitaelezea hivi punde.

Aidha, Sheria mpya ya Kodi ya Mapato iliyotungwa na Bunge hili Tukufu mwezi Aprili, 2004 itaanza kutumika mwezi Julai, 2004 kama ilivyopangwa. Zoezi la kutayarisha Kanuni za Sheria hii pamoja na maelezo ya kina ya vifungu mbalimbali vya sheria hiyo linaendelea vizuri. Sheria hiyo inatarajiwa kupanua wigo wa kodi na kuanzisha utaratibu mpya wa walipa kodi kujikadiria kodi wenyewe. Aidha, Idara ya

Walipa Kodi Wakubwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania imeimarishwa na malalamiko yaliyokuwepo ya walipa kodi hao yamepungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaelezea hapo awali, mwenendo wa upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu umekuwa wa kuridhisha kwa mwaka huu wa fedha wa 2003/2004. Katika kipindi cha Julai, 2003 hadi Mei, 2004 jumla ya misaada na mikopo kwa ajili ya Bajeti ya kawaida ilifikia shilingi milioni 490,253 sawa na asilimia 121 ya makisio tuliyojiwekea ya shilingi milioni 405,047. Fedha hizi pia zilitolewa mapema ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo hadi kufikia Desemba, 2003, asilimia 90 ya fedha hizo ilikwishapatikana na hivyo kutoa mchango mkubwa kwa Serikali katika kukabiliana na matatizo ya kibajeti yaliyotishia kujitokeza kutokana na ukame.

Mafanikio yote haya ni matokeo ya utekelezaji wa mkakati wetu wa kupokea misaada na mikopo *(Tanzania Assistance Strategy - TAS)* na wa kurahisisha utawala wa misaada *(Aid Harmonisation)* ili kupunguza urasimu na umimi kama ilivyo kuwa huko nyuma. Utaratibu huu pamoja na ule wa kujadiliana na Wafadhili katika vikao vya pamoja na pia kujadili matumizi ya Bajeti hadharani kila mwaka umeimarisha sana imani ya wafadhili kwa Tanzania kuliko nchi nyingi Afrika. *(Makofi)*

Pamoja na uhusiano huo unaoivumisha Tanzania katika duru za wafadhili, bado tunalo tatizo la kuimarisha zaidi uhuru wa Tanzania kuelekeza misaada hiyo kikamilifu na bado liko tatizo kubwa zaidi kuwa nchi karibu zote zingali bado kutimiza ahadi zao za kuongeza misaada chini ya makubaliano ya Monterrey, Mexico ili ifikie asilimia 0.7 au zaidi ya Pato la Taifa la nchi tajiri katika kutekeleza Mkakati wa Kuondoa Umaskini Duniani Karne hii *(Millenium Development Goals).* Tunazipongeza hasa Serikali za Uingereza na Ufaransa kwa kuongoza mijadala ya suala hili kwenye vikao vya Kimataifa na hata kupendekeza kuanzishwe Mfuko Maalum wa Kimataifa wa kuziwezesha nchi maskini sana duniani kupata misaada zaidi ya kupambana na umaskini jambo ambalo baadhi ya wakubwa wenzao wanalichenga au wanalikwepa kwa kuanzisha mifuko yao ya aina aina isiyolenga kikamilifu kukabiliana na umaskini kwa misingi iliyo kubalika tayari duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendeleza majadiliano na wafadhili mwaka ujao wa fedha kuhakikisha kuwa misaada na mikopo nafuu inaelekezwa katika maeneo yanayolenga kutekeleza dira na matakwa ya nchi *(complete ownership of aid utilization)* ili kukuza uchumi, hususan kwenye kilimo, elimu, viwanda na miundombinu, hasa madaraja na barabara za lami za kuunganisha Wilaya, Mikoa, Mikoa na Mikoa, maeneo ya uzalishaji mkubwa na baina yetu na nchi majirani. Maeneo haya ndiyo yatatuondoa kwenye ujinga na umaskini kwa haraka zaidi kuliko mengineyo ambayo ni ya ulaji *(consumption)* kuliko uzalishaji *(production).* Kupanga ni kuchagua pale panapoweza kulivusha Taifa letu haraka haraka. Tutaweza kulima kwa wingi, kusindika mazao hayo kwa wingi na kusafirisha mazao ya kilimo na viwanda hadi nchi jirani za kanda na ng'ambo kwa barabara za kuaminika hadi bandarini au nchi majirani hasa Kaskazini, Magharibi na Kusini mwa Tanzania. Hatuwezi kufanya hayo na mengineyo bila kuwa na

wasomi wa nyanja zinazoendana na ulimwengu huu wa elimu ya juu, sayansi na utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, napenda kuchukua nafasi hii kushukuru nchi wafadhili, Jumuiya ya Ulaya, pamoja na Mashirika yote ya Kimataifa yaliyotoa fedha kusaidia Bajeti yetu kwa mwaka huu wa fedha. Nchi na mashirika hayo ni Austria, Australia, Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, Ireland, Italia, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ubeligiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB), BADEA,* Benki ya Dunia, *EIB,* Jumuiya ya Ulaya, *Kuwait Fund, NDF, OPEC Fund* na Taasisi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kudhibiti ukuaji holela wa madeni chini ya Mkakati wa Madeni wa Taifa. Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Mwaka 1974 pamoja na marekebisho ya mwaka 2003 inaendelea kutekelezwa kikamilifu. Kwa sasa, mikopo inatafutwa kutoka vianzio vyenye masharti nafuu sana na kuelekezwa kwenye maeneo muhimu ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Aidha, udhamini wa Serikali kwa mikopo ya nje umesitishwa na hakuna ruksa kwa mtumishi au mamlaka yoyote kukopa kwa niaba ya Serikali au kufikia mapatano yanayohusu fedha bila idhini rasmi ya Waziri wa Fedha ambaye naye lazima ashauriwe kwanza na Kamati iliyoundwa chini ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kupata misamaha ya madeni toka nchi wanachama na zile zisizokuwa wanachama wa Kundi la Paris kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa katika mpango wa kuzipunguzia madeni nchi masikini. Nchi za Kundi la Paris, isipokuwa Brazil, zimefuta sehemu kubwa ya madeni yetu kwao na nyingine zimeyafuta kabisa madeni hayo. Nashukuru kwamba wiki iliyopita Rais wa Brazil alipokutana na Rais wetu walikubaliana kwamba hatua za haraka zitachukuliwa kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Juhudi za kufanya majadiliano na Brazil zitaendelea mwaka ujao wa fedha. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, tumepata msamaha wa deni kiasi cha dola za Marekani milioni 15.1 toka Bulgaria na mazungumzo ya awali yamekamilika kwa Iran na karibu kukamilika kwa Mfuko wa Abu Dhabi na mashirika ya kibiashara ya India ambayo tayari imetufutia madeni ya Kiserikali. *(Makofi)*

Juhudi zitaendelea kuwa na mazungumzo na nchi nyingine zinazotudai ili zitufutie madeni kwa mujibu wa makubaliano ya Kimataifa kwa nchi maskini sana duniani. Majadiliano na nchi na mashirika yasiyo ya Kundi la Paris yamekuwa magumu kwa wao kutokubali kutii makubaliano ya Paris, suala linalo zua mijadala katika mikutano ya Kimataifa ambapo baadhi ya nchi zimeshitakiwa na mali zao kufilisiwa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu wa fedha unaonyesha kwamba kwa kiasi fulani kumekuwa na ongezeko la ufanisi na udhibiti wa matumizi hasa katika Serikali Kuu kama ilivyo kwenye ukusanyaji wa mapato. Hii inamaanisha kwamba Serikali inaanza kuona matunda (ingawa ya awali) ya hatua ilizochukua kwa kipindi cha miaka minane iliyopita za kupanga na kusimamia Bajeti,

kuondoa matumizi yasiyo ya lazima na kujifunza kutumia kile tulicho nacho. Ni ishara nzuri pia kwamba sasa taratibu na kanuni za ununuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma (Na. 3 ya 2001) zinaeleweka.

Aidha, licha ya matumizi makubwa yaliyosababishwa na ukame katika maeneo ya chakula na umeme, matumizi ya Serikali kwa ujumla yamedhibitiwa na hakuna athari kwenye Bajeti ya mwaka huu. Serikali imehakikisha kwamba sekta za kuondoa umaskini yaani Afya, Elimu, Maji, Barabara, Kilimo, Mahakama na sheria zimepata fedha kulingana na Bajeti zao hata pamoja na kwamba kumekuwa na matumizi makubwa kwa ajili ya *TANESCO* na chakula. Kigezo kikubwa cha uimara wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu ni kwamba Serikali haikukopa kutoka Benki Kuu nje ya lengo. Badala yake hata kiwango cha kukopa Benki Kuu kilichowekwa katika makubaliano yetu na *IMF* chini ya mpango wa *PRGF,* hakikuvukwa. Hili limewezekana kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, misaada ya Bajeti kutoka kwa nchi wafadhili ambayo pia imepita lengo kidogo, udhibiti wa matumizi ya Serikali na kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Katika kipindi cha Julai, 2003 hadi Machi, 2004, matumizi kwa ujumla yalifikia shilingi trilioni moja, bilioni mia saba ishirini na mbili na mia sita kumi na mbili milioni (1,722,612 milioni) ikilinganishwa na makisio ya shilingi trilioni moja, bilioni mia nane themanini na tisa na milioni mia mbili na saba (1,889,207 milioni) katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 422,559 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi trilioni moja, bilioni mia tatu na milioni hamsini na tatu (1,300,053 milioni) ni kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba kutokana na hali ya ukame ulioikumba nchi yetu mwaka 2003, Serikali ililazimika kuandaa Bajeti ya Ziada na kupata kibali cha Bunge cha kutumia fedha kiasi cha shilingi milioni 176,784 zaidi ya zilizoidhinishwa awali katika bajeti ya 2003/2004. Mahitaji ya nyongeza ya shilingi milioni 176,784 yalikuwa ni pamoja na ununuzi na usambazaji wa chakula cha njaa, msaada kwa *TANESCO* kuiwezesha kumudu gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta badala ya nguvu za maji, fidia kwa Halmashauri za Wilaya na Miji kufuatia kufutwa kwa kodi zenye kero, mchango katika Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali pamoja na malipo kwa Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF),* kufidia michango ambayo haikuwa imewasilishwa na mashirika hayo kabla ya kubinafsishwa. Mahitaji mengine ya ziada yalihusu maandalizi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ukaguzi wa dhahabu na ununuzi wa ndege mpya ya Serikali. Mahitaji haya yaligharamiwa kwa njia mbili; kwanza, shilingi 87,250 milioni zilitokana na mapato mapya na pili, Shilingi 89,534 milioni zilitokana na uhamisho wa fedha ambazo zilikuwa ndani ya bajeti iliyokwishaidhinishwa. Matumizi hayo ya nyongeza yalifanyika na yanaendelea kufanyika kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na mwenendo wa mapato na matumizi hadi sasa inatarajiwa kwamba kwa mwaka wote wa fedha mapato yatavuka lengo kwa shilingi 74,210 milioni sawa na asilimia 5.3 zaidi ya lengo. Inategemewa pia kwamba misaada na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya Bajeti nayo itazidi lengo. Mapato kutokana na

ubinafsishaji ambayo yalikadiriwa kufikia shilingi bilioni17bn/= yaelekea hayatapatikana yote.

Kuhusu malengo ya matumizi, mwelekeo ni kwamba, maeneo mengi ya matumizi ya maendeleo na ya kawaida hususan Matumizi Mengine *(OC)* hayatafikia malengo kwa sababu zilizoelezwa awali. Aidha, kuna mwelekeo wa malengo kufikiwa katika sekta za kipaumbele za kupunguza umaskini na kukuza uchumi.

Ili kuendelea kuboresha usimamizi wa fedha za umma, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na kuanzisha Kamati za ukaguzi wa ndani wa hesabu za Serikali katika Wizara, Idara na Wakala zote za Serikali. Mafunzo hivi sasa yanaendelea ya kuelimisha Wakaguzi hao kuhusu kazi za Kamati hizo. Kanuni na taratibu za ukaguzi wa ndani wa hesabu zimekamilishwa na zitachapishwa hivi punde na kutangazwa kwa wadau wote. Aidha, Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa *(NAO)* inaimarishwa kwa kupatiwa makao mapya ya ofisi, na sasa inakamilisha mpango wa kurekebisha muundo wake wa ndani na kujaza nafasi za kazi zilizo wazi ili kuongeza tija katika utendaji wake. Vile vile, maandalizi yamekamilika ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 3 ya 2001 ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali, hasa kuhusu miradi ya maendeleo. Marekebisho hayo yatawasilishwa katika Kikao hiki cha Bunge kwa kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya huduma za kibenki, kuna maendeleo ya kuridhisha pia. Ujazi wa fedha ulidhibitiwa na kuongezeka kwa asilimia 18.7 kati ya Julai 2003 na Machi 2004 kulinganisha na asilimia 22.7 mwaka uliotangulia. Mwenendo huu wa ujazi wa fedha unathibitisha kwamba tumeweza kweli kuweka msingi thabiti wa kuzuia mfumuko wa bei. Mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 41.8 kati ya Julai 2003 na Machi 2004. Ongezeko hili limetokana hasa na kampuni kubwa hapa nchini kuacha kukopa kutoka benki za nje ya Tanzania, badala yake sasa zinakopa kutoka benki za hapa nchini. Hali hii inatokana na sababu kadhaa, kubwa zikiwa, kwanza kuepuka hasara inayotokana na kubadilika kwa bei ya fedha za kigeni *(Exchange Rate)* ; na pili kushuka kwa gharama za kukopa hapa Tanzania hasa kutokana na ongezeko la ushindani katika sekta ya kibenki.

Kwa hiyo, riba ya mikopo sasa imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 13.5. Riba ya amana kwa upande mwingine imepanda na kufikia wastani wa asilimia 4.1. Sasa tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana imeshuka kutoka kiwango cha 10.6 mwezi Juni 2003 hadi 9.4 mwezi Machi 2004. Ingawa riba ya amana bado ni ndogo na ile ya mikopo bado ni kubwa, mwenendo huu unatia moyo na ni dalili nzuri kwamba benki sasa zimepata uelewa mkubwa wa soko la Tanzania, hasa mahitaji ya huduma za benki na kwamba riba zitaendelea kubadilika kulingana na mahitaji ya soko. Serikali inaamini kwamba hili litatokea kwa kuzingatia mabadiliko ambayo Serikali imefanya ili kuboresha mazingira yanayotoa motisha kwa benki kama vile kurekebisha Sheria ya Ardhi, kuimarisha Kitengo cha Mahakama Kuu kinachoshughulikia Mashauri ya Biashara, kuanzisha mifuko ya kudhamini mikopo *(Credit Guarantee Schemes)* na maendeleo yanayotokea katika miundo mbinu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa urari wa malipo ya nje *(Balance of Payments),* kumekuwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa kutoka nje, na pia ongezeko la mauzo ya nje, hasa ya bidhaa zisizo asilia. Uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka kwa asilimia 26.6 katika mwaka wa 2003, kutokana na mafuta ya petroli na chakula na hasa mchele. Uagizaji wa mafuta ya petroli umeongezeka kutokana na mahitaji makubwa ya *TANESCO* kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kutumia mitambo ya mafuta badala ya maji. Usafirishaji nje wa bidhaa uliongezeka kwa asilimia 16 ukitokana hasa na dhahabu na bidhaa za viwandani. Usafirishaji wa mazao asilia uliendelea kuzorota ingawa kuna dalili za kupanda tena kwa bei za kahawa, pamba, chai, na korosho katika soko la dunia. Mapato yatokanayo na Utalii yaliongezeka katika Mwaka huu. Kwa ujumla, kwa mara ya kwanza, urari wa malipo ya nje ulikuwa na ziada (surplus) ya dola za Marekani 243.9 milioni. Kwa kuzingatia misamaha ya Madeni na ongezeko la misaada na mikopo ya bajeti, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani 1,973.2 milioni (dola bilioni moja milioni mia tisa sabini na tatu na laki mbili) sawa na shilingi trilioni 2.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa tunapata mafanikio makubwa kutokana na marekebisho ya sera na utawala, bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuweza kujitegemea na la muhimu zaidi kuondoa umaskini. Baadhi ya mambo mengine muhimu yaliyo jitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu wa fedha unaoisha ni:-

(i) Bajeti ya Serikali bado ni tegemezi kwa kiasi kikubwa, ingawa kiwango cha utegemezi kinapungua. Katika mwaka 2003/2004, Wafadhili pamoja na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa wamechangia asilimia 45 ya Bajeti ya Serikali ikilinganishwa na asilimia 47 mwaka 2002/2003. Hivyo, ingawa mapato ya ndani yanaongezeka, pengo la kujitegemea bado ni kubwa.

(ii) Pamoja na kupewa upendeleo maalum, fedha zinazotengwa kwa sekta za kuondoa umaskini bado hazitoshelezi mahitaji.

(iii) Ingawa ufanisi na nidhamu Serikalini vimeongezeka kiasi, uwezo wa utendaji hasa katika maeneo ya uhasibu, mawasiliano, utibabu na kadhalika bado ni duni na ndio sababu miradi ya maendeleo haitekelezwi kwa wakati na hata hesabu za Serikali haziko sahihi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 unazingatia malengo muhimu ya uchumi ambayo ni pamoja na:-

(i) Uchumi kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2004 na asilimia 6.5 mwaka 2005. Kukua huku kutatokana na kilimo, uzalishaji viwandani na uzalishaji kwa mauzo ya nje.

(ii) Mapato ya ndani yanalengwa kufikia shilingi trilioni moja, bilioni mia saba thelathini na tisa na milioni mia mbili themanini na nane (1,739,288 milioni) sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa.

(iii) Mfumuko wa bei utakuwa katika kiwango cha asilimia nne ifikapo Juni 2005 na baadaye kulingana na viwango vya wastani katika nchi tunazofanya nazo biashara na zile tunazoshindana nazo katika biashara ya nje.

(iv) Akiba ya fedha za kigeni inalengwa iwe katika kiwango ambacho kinatosha kulipia mahitaji muhimu ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa muda usiopungua miezi sita.

(v) Kupunguza kiwango cha utegemezi wa bajeti ya Serikali hadi asilimia 41 mwaka 2004/05.

(vi) Kusimamia utekelezaji wa sera ya mikopo midogo midogo *(Micro-finance)* na mpango wa dhamana kwa wawekezaji wadogo wadogo *(Small and Medium Scale Enterprises (SMEs)* na miradi mikubwa ili kuwezesha wananchi walio wengi kujiendeleza kiuchumi kwa kujipatia mikopo zaidi ya kibenki.

Mheshimiwa Spika, muhula wa kwanza wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini umemalizika na taarifa ya tatu ya utekelezaji wa Mkakati huo imechapishwa. Taarifa hiyo imeainisha matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu hali ya umaskini nchini. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayesimamia Mkakati wa kuondoa umaskini ataelezea kwa kina maudhui ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo imebainisha, pamoja na mambo mengine, kwamba maendeleo ya kilimo ambayo ni sekta muhimu kuliko zote Tanzania yanakwamishwa na mambo mengi. Vikwazo hivyo ni pamoja na ukosefu wa mikopo ya pembejeo na mitaji, ukosefu wa huduma za ugani, mazingira mabaya ya uwekezaji, ubovu wa miundombinu na mengine mengi. Wakati huo huo, sekta ya kilimo bado inabakia kuwa sekta kuu katika uchumi wa Tanzania. Udogo wa mashamba, teknolojia duni na utegemezi kwa mvua ni baadhi ya orodha ya matatizo yanayokwamisha maendeleo ya kilimo na pia maendeleo ya wananchi wanaokitegemea. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali kila mwaka katika jitihada za kuondoa matatizo haya lakini hayajatokomezwa bado.

Mheshimiwa Spika, ili kuinua kilimo, Serikali imechukua hatua za ziada zenye lengo la kuvutia uwekezaji katika sekta hii, na papo hapo kuwezesha wakulima wadogo kuongeza tija ya jasho lao, na kujiondolea umaskini. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Moja, chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004:

(a) Kuna punguzo la mara moja asilimia mia moja (100% *Capital Expensing)* la gharama za kusafisha pori, ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji, kupanda mazao ya kudumu na kutunza mazingira au kudhibiti mmomonyoko katika ardhi inayotumika kwa kilimo. Kwa taratibu za kawaida za kiuhasibu, gharama hizi ni za rasilimali *(Capital Expenditures)* na zingepunguzwa kwa kipindi kirefu sana, sasa zitapunguzwa mara moja. *(Makofi)*

(b) Gharama ambazo mtu ametumia kuhifadhi mazingira kwenye ardhi inayotumiwa kwa kilimo, ufugaji wa wanyama au samaki, au kuirejeshea ardhi hiyo hali yake baada ya kuharibiwa, zinapunguzwa katika kukadiria mapato ya mhusika kwa minajili ya kodi ya mapato. *(Makofi)*

(c) Gharama za utafiti na uendelezaji wa mashamba ya kilimo na mifugo zinapatiwa punguzo hilo kwa ajili ya kodi ya mapato.

(d) Vifaa vya umwagiliaji maji mashambani vimeingizwa katika kundi moja na magari makubwa ili kupata punguzo la uchakavu kwa kiwango cha juu zaidi cha asilimia 25 kwa mwaka. *(Makofi)*

(e) Matrekta na mitambo mingine inayotumiwa katika kilimo, ufugaji na uvuvi imeingizwa katika kundi la mitambo ya viwandani na kupatiwa punguzo la uchakavu la asilimia 50 katika mwaka wa kwanza na asilimia 25 miaka inayofuata. *(Makofi)*

(f) Wafanyabiashara wa mazao ya kilimo kwa maana pana yaani kilimo, uvuvi na mifugo hawatakiwi kulipa kodi ya awali kwa awamu sawa *(equal quarterly instalments),* bali mwisho wa robo ya tatu ya mwaka baada ya kuvuna.

Mbili, chini ya Sheria ya Ushuru wa Forodha, zana na pembejeo za kilimo kama vile matrekta, madawa ya kuua wadudu na mbolea hivi sasa hazitozwi Ushuru wa Forodha. Ikiwa kuna kodi zilizosalia bado katika maeneo haya zitafutwa. *(Makofi)*

Tatu, chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*:-

(a) Mazao ghafi ya kilimo na mifugo yanapata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* ikiwa ni pamoja na nyama isiyosindikwa, mazao ya mifugo ambayo hayajasindikwa, samaki zisizosindikwa na mazao mengine yote ya kilimo ambayo hayajasindikwa. *(Makofi)*

(b) Hakuna Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye pembejeo za kilimo na uvuvi kama vile madawa ya kuua wadudu, mbolea, madawa na vifaa vya mifugo, vifaa vya kilimo kama matrekta, majembe, sururu, nyavu, mashine na vifaa vya uvuvi. *(Makofi)*

(c) Kuna unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* pia kwa mazao ya kilimo yanayouzwa nje na wakulima waliojiunga kwenye Vyama Vya Ushirika au Umoja wa Wazalishaji *(Associations)* na kujisajili chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. *(Makofi)*

Nne, chini ya Sheria ya Ushuru wa Stempu, mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yamesamehewa ushuru wa stempu. Aidha, ushuru wa stempu haukusanywi katika magulio, ambapo mazao haya huuzwa kwa wingi. *(Makofi)*

Tano, chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa:-

(a) Bado sheria inakataza Serikali za Mitaa kutoza kodi inayozidi asilimia tano (5%) ya bei ya shambani au Chama cha Msingi au cha wakulima kwenye mazao ya kilimo, hili tuliliamua mwaka jana. Aidha, kodi hiyo inatakiwa kutozwa pale ambapo mazao husika yamelimwa au yanaponunuliwa kwa mara ya kwanza kutoka kwa wakulima na siyo katika Wilaya yanakopitia yakielekea sokoni au Wilaya nyingine au nchi hata nchi jirani. *(Makofi)*

(b) Kodi na ada zinazoruhusiwa kutozwa ni zile tu zilizoorodheshwa katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Fedha ya Taifa ya mwaka 2003. *(Makofi)*

Sita, katika Bajeti ya Matumizi ya Serikali:-

(a) Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kilimo katika ngazi ya Wilaya. *(Makofi)*

(b) Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufidia gharama za usafirishaji wa mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa mingine yenye mvua za uhakika itakayotangazwa na Waziri wa Kilimo na Chakula, yeye ndiye anaijua Mikoa hiyo. *(Makofi)*

(c) Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Vyama vya Ushirika na vyombo vingine vinavyonunua mazao ya wakulima utaimarishwa kwa kuongezewa fedha katika bajeti hii. Mfuko huu umekuwa na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kufuta kodi au kutoa unafuu mkubwa wa kodi na fidia ya mbolea iliyotangazwa mwaka tunaomalizia kwa wakulima, wafugaji na wavuvi, hasa wadogo na wa kati ambao wengi ni wananchi zikiunganishwa na mpango wa Serikali wa kudhamini wakulima wadogo wadogo ili waweze kukopa kutoka mabenki kibiashara na mipango inayoendelea ya kuchimba na kuimarisha barabara Vijijini hadi Taifani, na pia hatua za kuondoa kero za kodi za leseni ambazo nitazitangaza hivi punde ni ushahidi imara wa utekelezaji wa sera na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hatua madhubuti za kuwawezesha Watanzania Vijijini kuzalisha mali na kujitajirisha kwa kujituma na kuwa wabunifu, ni msumari muhimu kwenye jeneza la kuuzika umaskini kisayansi. Atakayesema kwamba Bajeti hii haimsaidii maskini au mkulima, mfugaji na mvuvi atakuwa anapotosha tu ukweli. Aliye na macho haonyeshwi njia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, hatua za kuimarisha na kuboresha vyanzo vya akiba za pamoja za wananchi zitachukuliwa, ambapo *"Unit Trust of Tanzania" (UTT)* itauza hisa *(Units)* kwa wananchi. Uanzishwaji wa *'Collective Investment Schemes'* ambapo wananchi watashirikiana kuweka akiba kwa pamoja na hivyo kushiriki katika masoko ya mitaji nchini litakuwa jambo geni sana.

Mheshimiwa Spika, *UTT* itashirikiana pia na benki za biashara katika kuanzisha chombo cha kuweka kumbukumbu za wakopaji *(Credit Reference Bureau)* ili kuboresha

mazingira ya benki kukopesha. Aidha, hatua zinazochukuliwa kuimarisha mifuko ya dhamana ya mikopo na mitaji zinalenga pia kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi trilioni moja, bilioni mia saba thelathini na tisa na milioni mia mbili themanini na nane (milioni 1,739,288) sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa.

Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 20 ikilinganishwa na mapato yanayotarajiwa kukusanywa mwaka huu wa 2003/2004. Azma ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 na muda wa kati ujao itaendelea kuwa ya kuongeza mapato, kupunguza utegemezi, kugharamia mpango wa kuondoa umaskini na kuhakikisha kwamba hatubebi tena mzigo tusiouweza wa madeni. Hatua kuu zitakazochukuliwa katika kuongeza mapato ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha usimamizi na utawala wa Mamlaka ya Mapato, hasa kwa kupanua Idara ya Walipa Kodi Wakubwa.

(ii) Kutekeleza Sheria Mpya ya Kodi ya Mapato ya 2004 na kukamilisha mapitio ya Sheria nyingine za Kodi kwa lengo la kuziboresha.

(iii) Kuanza utekelezaji wa Mkataba wa Kuanzishwa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki.

(iv) Kuingiza mapato yatakayotokana na mauzo ya gesi ya Songo Songo katika maduhuli ya Serikali. Mategemeo ni kwamba gesi hii itaanza kupatikana kunako mwezi Julai 2004.

(v) Kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika baadhi ya maeneo ili kuuboresha zaidi pamoja na kuweka vivutio kwa baadhi ya sekta ili kukuza Pato la Taifa.

(vi) Kuimarisha makusanyo ya mapato kutoka Wizara na Idara, hasa zile zilizo kwenye utaratibu wa *"retention"*.

(vii) Kusimamia kikamilifu biashara ya bidhaa ya mafuta ya petroli ikiwemo kufungwa kwa *"Flow Meter"* bandarini ili kudhibiti ukwepaji kodi. *"Flow Meter"* inategemewa kufungwa mwezi Julai, 2004.

(viii) Kuendeleza utaratibu wa utawala wa misamaha ya kodi kwa njia ya *"Treasury Voucher"* na kuangalia uwezekano wa kuingiza katika utaratibu huu vifaa vinavyoingizwa nchini kwa miradi inayogharamiwa na Wafadhili.

(ix) Kuimarisha utendaji wa *TRA* kwa kuongeza matumizi ya teknolojia, tija ya watumishi, mafunzo na huduma bora kwa walipa kodi.

(x) Kuanzia Julai 2004 ukaguzi wa mizigo utafanywa baada ya kuwasili nchini, kitu kinachoitwa *destination inspection* badala ya utaratibu wa sasa wa kukagua kabla ya kuwasili *(Preshipment Inspection).* Utaratibu huu utaboresha mazingira ya biashara, utaondoa kero kwa waagizaji wa bidhaa na utaboresha mazingira ya uwekezaji.

(xi) Kuongeza saa za kazi za shughuli za forodha ili kuondoa msongamano wa mizigo bandarini. Vyombo vyote vinavyotoa huduma katika maeneo ya Forodha vitatakiwa kushirikiana kwa karibu zaidi na Idara ya Forodha ili kufanikisha azma hii ya kuongeza saa za kazi. *(Makofi)*

(xii) Zoezi limeanza la kuainisha maeneo ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ambayo yanahitaji kurekebishwa ili kuondoa mianya ya ufujaji wa mapato ya Serikali.

(xiii) Imeundwa Kamati ya kutathmini sheria na kanuni zinazotawala uwekezaji katika sekta ya madini kwa lengo la kutoa mapendekezo ya kuziboresha ili Serikali isipoteze yale mapato ambayo ni halali yake.

Mheshimiwa Spika, inaeleweka wazi kuwa misaada kutoka nje sio njia nzuri ya kuendeleza uchumi imara na wa kudumu *(Sustainable Economy).* Hata hivyo katika kipindi hiki ambacho tunafufua uchumi wetu na kuondoa umaskini, michango ya Wafadhili ni muhimu katika kusaidia Serikali yetu.

Sera safi tulizo nazo pamoja na usimamizi imara wa uchumi vimewezesha Wafadhili na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kupenda kuendelea kutoa misaada yao kuchangia bajeti ya Taifa. Kama nilivyosema awali, ni muhimu kutumia nafasi hii vizuri na kuhakikisha kuwa michango hii inatumika vizuri kutuwezesha kuondoa umaskini na kuleta maendeleo kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi za Bara la Asia.

Mkakati wetu wa Kusimamia Misaada *(Tanzania Assistancy Strategy)* utazidi kutuongoza ili kuhakikisha misaada na mikopo ya masharti nafuu inatumika vizuri kukuza uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majadiliano tuliyofanya na nchi Wafadhili na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, katika mwaka wa fedha 2004/2005, tunatarajia kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu kiasi cha shilingi trilioni moja, bilioni mia tatu sitini na saba na milioni ishirini na tano(Shilingi 1,367025 milioni) ambacho kitakuwa asilimia 41 ya matumizi yote ya Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi 509,140 milioni ni misaada ya Bajeti na shilingi 857,885 milioni (857,885,000,000/=) ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kiwango hiki cha misaada na mikopo kinaonyesha ongezeko la shilingi 191,204,000,000 au asilimia 16 ikilinganishwa na matarajio ya misaada na mikopo kwa mwaka huu wa fedha wa 2003/2004. Ni mategemeo yetu kwamba Nchi Wafadhili zitaendelea kuongeza misaada yao kwa Tanzania na kutekeleza kikamilifu ahadi za *Monterrey (Monterrey Consensus),* ya kuhakikisha kuwa tunawezeshwa kufikia

malengo ya Maendeleo ya Milenia Mpya *("Millenium Development Goals" - MDGs).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia akiba yake Benki Kuu pamoja na kukopa katika vyanzo vya ndani kiasi cha shilingi 231,110,000,000 kwa kutumia dhamana za muda mfupi na mrefu.

Sehemu kubwa ya mikopo hiyo itatumika kulipia madeni yaliyoiva *(rollover)* na madeni mengine yanayotokana na Mikataba. Kiasi kingine kitatumika kuchangia mfuko wa dhamana ya mikopo kwa bidhaa za kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imedhamiria kuendelea kusimamia vyema nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mtandao wa kompyuta wa kutayarisha na kutekeleza bajeti ya Serikali. Hatua hii ni pamoja na kupanua teknolojia hii ili ifike kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha kwa mwaka 2004/2005 umezingatia mambo yafuatayo:-

(i) Sekta za kipaumbele katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini zimeendelea kupewa upendeleo. Hata hivyo kwa kuzingatia mahitaji mapya ya fedha kugharamia matayarisho ya Uchaguzi Mkuu na pia mahitaji ya sekta ya nishati, hasa kuhusu umeme, nyongeza katika sekta hizo za kuondoa umaskini haitakuwa kubwa, isipokuwa kwa zile ambazo zinapata misaada mikubwa ya Wafadhili.

(ii) Utaratibu wa kutoa ruzuku, kupunguza gharama za usafirishaji wa mbolea kwenda Mikoa iliyoteuliwa utaendelezwa mwaka huu wa 2004/2005. *(Makofi)*

(iii) Utaratibu wa kutoa fedha kulingana na mapato yaliyopo *(Cash Budget)* utaendelea.

(iv) Fedha zaidi zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wauzaji wa bidhaa nchi za nje *(Export Credit Guarantee Scheme)* na Mfuko wa Dhamana kwa Biashara ndogo na za kati *(Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme).*

(v) Mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya kwa utaratibu wa angalau zao moja la chakula na zao moja la biashara utaendelezwa.

(vi) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia juhudi za Serikali za kutumia mapato yake ya ndani katika ujenzi wa barabara muhimu. Mwaka 2004/2005, Serikali itaendelea na utaratibu huo ambapo fedha zaidi ya zile zilizotolewa mwaka huu zimetengwa, kama atakavyoeleza zaidi Waziri wa Ujenzi atakapo-wasilisha Bajeti ya Wizara yake baadaye.

(vii) Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha mishahara ya watumishi wake, ili kufikia asilimia 4.8 ya Pato la Taifa kama ilivyodhamiriwa katika mpango huo. Aidha, Serikali inaandaa utaratibu maalum wa kushughulikia kwa haraka malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Serikali wakiwemo walimu. Malipo ya malimbikizo hayo yalisitishwa kutokana na matukio ya wizi wa kalamu wa mishahara ulio fanywa na watumishi wachache wasioaminika ambao sasa umefanyiwa uchunguzi na hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wanaohusika. *(Makofi)*

(viii)Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mikubwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Umuhimu wa kwanza unawekwa kwa miradi ambayo tayari ina mikataba.

(ix)Bajeti imeendelea kutenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada (grants) isiyo ya miradi kwa ajili ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Utaratibu huu utaendelea hadi hapo mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* yatakapopatikana.

(x)Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali itawarejesha katika Daftari la Pensheni wastaafu waliokuwa wamepokea mafao yao kwa mkupuo. Wastaafu hawa wanategemewa kuanza kupokea malipo yao mwezi Januari, 2005, ili kujipa muda wa matayarisho baada ya sheria husika kurekebishwa. *(Makofi)*

(xi)Kutokana na ongezeko la matukio ya ujambazi nchini, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka ujao na vitendo vingine vya uhalifu, bajeti ya mwaka 2004/2005 imeongeza mgao wa fedha kwa vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

(xii) Katika mwaka 2004/2005, Serikali imetenga fedha zaidi kwa ajili ya chakula cha dharura endapo hali ya hewa itakuwa mbaya pamoja na kugharamia Mfuko wa Hifadhi ya Chakula *(SGR)*. *(Makofi)*

(xiii)Kama ilivyokuwa katika mwaka 2003/2004, Bajeti ya 2004/2005 imetenga fedha kwa ajili ya kulipia mahitaji ya sekta ya Nishati na hasa *TANESCO* kuisaidia katika mpango wake wa dharura, pamoja na malipo ya *Capacity Charge* kwa *IPTL* na *Songas*.

(xiv)Kwa kuzingatia ukweli kuwa idadi ya Wabunge inategemea kuongezeka baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani, Mifuko ya Hifadhi za Jamii imekubali kwa ridhaa yao wenyewe, kujenga Ukumbi mpya kwa utaratibu wa kujenga, kukodisha na hatimaye kuikabidhi Serikali. Kwa sababu hii, mradi huu hauko kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka huu lakini utatekelezwa kwa mpango huo niliooueleza. Serikali pia inafikiria kutumia utaratibu kama huu kwa miradi mingine mikubwa ya ujenzi ikiwemo miradi ya barabara. *(Makofi)*

(xv)Kwa kuzingatia umuhimu wa michezo, Bajeti ya mwaka 2004/2005 imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa. Sehemu kubwa ya fedha

hiyo ni msaada wa Serikali ya China. Na kwa mujibu wa mkataba ujenzi huo utaanza mwezi Septemba, 2004. *(Makofi)*

(xvi) Mgao wa Ruzuku kwa Halmashauri za Wilaya kwa mwaka 2004/2005 umezingatia utaratibu mpya ambao umebuniwa kufuatia zoezi la kina lililoshirikisha wadau wa aina zote. Utaratibu mpya umetumika katika kutenga fedha za bajeti ya kawaida kwa sekta za afya na elimu kwa Halmashauri, na umetumika kwa sekta zote katika fedha za bajeti ya maendeleo. Utaratibu huu mpya unajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu usawa wa mgao wa bajeti Kimkoa na Kiwilaya. Maelezo zaidi yatatolewa na Waziri wa TAMISEMI atakapowasilisha bajeti ya Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Makisio ya Bajeti ya Mwaka 2004/2005. Kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali imelenga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni moja, bilioni 739 na milioni 288 (1,739, 288 milioni) mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa msingi wa mfumo wa kodi wa sasa, pamoja na marekebisho yanayopendekezwa katika eneo la kodi. Kiwango hiki cha mapato ni sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa. Serikali inakusudia pia kuingiza katika mapato yake shilingi 10,115 milioni mapato yatakayotokana na uuzaji wa hisa za Serikali katika baadhi ya Mashirika ambapo Serikali ni mbia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni tatu, bilioni mia tatu arobaini na saba, milioni mia tano thelathini na nane (Shs. 3,347,538, milioni) katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Kwa kuzingatia mapato ya shilingi trilioni moja, bilioni mia saba thelathini na tisa, milioni mia mbili themanini na nane (Shs. 1,739,288 milioni) na yale ya kuuza hisa za shilingi bilioni kumi, milioni mia moja kumi na tano (Shs. 10,115 milioni), bajeti inakuwa na pengo la shilingi trilioni moja, bilioni mia tano tisini na nane, na milioni mia moja thelathini na tano (shs. 1,598,135 milioni). Sehemu kubwa ya pengo hili itajazwa na misaada ya Nchi Wafadhili, Jumuiya ya Ulaya, mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, hususan Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Kwa mujibu wa makubaliano tuliyofikia kati ya Serikali ya Tanzania na hawa Wafadhili na Mashirika kwa pamoja, tumekadiria kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu, jumla ya shilingi trilioni moja, bilioni mia tatu sitini na saba, milioni ishirini na tano (Shs. 1,367,025 milioni) mwaka wa 2004/2005. Kwa hiyo pengo linapungua hadi shilingi bilioni mia mbili thelathini na moja, milioni mia moja na kumi (Shs. 231,110 milioni). Pengo hili litazibwa kwa njia ya kupunguza akiba ya Serikali katika Benki Kuu na kukopa kutoka soko la fedha la ndani kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa kodi, ada mbalimbali na hatua nyingine za mapato. Hapo mwanzo nimetoa maelezo kuhusu matokeo mazuri ya hatua zilizochukuliwa na Serikali mwaka huu wa fedha unaoisha za kuongeza tija na kuziba mianya katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Aidha, kama nilivyoeleza awali, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuona kuwa tija katika sekta ya kilimo inaongezeka ili kupanua ajira, kujitosheleza kwa chakula,

kupunguza umaskini, na kuongeza mauzo yetu nje ya nchi. Pamoja na hatua mbalimbali zilizokwishachukuliwa, Serikali itachukua hatua za ziada mwaka wa fedha ujao yaani mwaka wa fedha ujao.

Serikali imeona kuna haja ya kutoa vivutio zaidi ili kuhamasisha uwekezaji wa miradi mikubwa na ya kati katika sekta hii ili kutumia ardhi kubwa ambayo hivi sasa haitumiki ipasavyo na kuongeza nafasi za ajira vijijini. Aidha, tunalenga kuongeza tija kwa viwanda vinavyozalisha pembejeo au kusindika mazao ya kilimo. Hatua hizo ambazo ni nyongeza ya zile nilizoelezea awali ni pamoja na hizi zifuatazo. Ni hatua mpya tena hizi:-

(a) Kwa Wakulima na Wafugaji Wakubwa:

(i)Katika Mfumo wa Kodi ya Mapato, utatolewa unafuu wa asilimia mia moja (100% expensing) ya gharama za mtaji katika mwaka wa kwanza wa kutumia rasilimali inayotokana na gharama hizo. Unafuu huu pia utahusu mitambo ya usindikaji wa mazao ghafi ya kilimo mashambani au uvuvi. Nia ni kuongeza uwekezaji katika teknolojia ya kilimo.

(ii)Katika Mfumo wa Ushuru wa Stempu, utawekwa ukomo wa Shilingi 500 kwa kiwango cha ushuru unaolipwa wakati wa kuhamisha milki (conveyance) ya ardhi ya kilimo pale watu wanapouziana ardhi. Nia ni kupunguza gharama za kubadilisha milki ya ardhi ya kilimo.

(iii)Katika Mfumo wa Tozo ya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(Skills Development Levy),* tozo hiyo kwa ajira za mashambani itafutwa. *(Makofi)*

(b) Kwa Wakulima na Wafugaji Wadogo Wadogo:

Hatua zilizotangazwa mwaka jana za kuboresha mazingira na mapato ya wakulima na wafugaji wadogo wadogo zinapaswa kutekelezwa kwa ukamilifu. Napenda kukumbusha kwamba Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zina fursa ya kutoza kodi na tozo zilizoorodheshwa katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kufuatia marekebisho yaliyofanywa mwaka jana.

Aidha, Halmashauri zinakumbushwa kuzingatia ukomo wa asilimia 5 ya bei ya mazao kwa mkulima kwa ajili ya Ushuru wa Mazao unaotozwa, na iwapo tu mazao husika yamezalishwa katika eneo la Halmashauri hiyo kama nilivyosema awali.

Aidha, imedhihirika kwamba Halmashauri nyingi bado zinatoza michango mabalimbali kwenye mazao kwa maelezo kuwa ni ya hiari! Inasisitizwa kwamba michango ya namna hiyo inakubalika tu pale ambapo wanakijiji wameshirikishwa na michango iwe kwa ajili ya miradi maalumu inayotekelezwa ndani ya kijiji husika au kwa ushirikiano wa vijiji kadhaa.

(c) Kwa Viwanda vya Pembejeo za Kilimo na Uvuvi:

Kwa kuwa pembejeo za kilimo na uvuvi hazitozwi *VAT,* wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo wanapata ushindani usio wa haki kutoka kwa bidhaa za namna hiyo zinazotoka nje. Ili kuondoa kasoro hii, inapendekezwa kuwa bidhaa husika zijumuishwe kwenye kundi la kutozwa *VAT* kwa kiwango cha sifuri *(zero rate)* zinapouzwa na wazalishaji wa ndani ili kuwawezesha wazalishaji hao kurejeshewa kodi wanayolipa kwenye nyenzo na malighafi. Aidha, hatua hii itaboresha mazingira ya uwekezaji kwa ajili ya kuzalisha pembejeo.

(d) Kwa Viwanda vya Mazao ya Kilimo na Uvuvi:

Pamoja na hatua zilizotangazwa chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato, inapendekezwa kuwa:

(i) Mvinyo na brandi vitakavyotengenezwa kutokana na zabibu za hapa nchini visitozwe Ushuru wa Bidhaa. Lengo ni kupanua soko la zabibu hapa nchini, ili kupanua kilimo cha zao hilo, hasa Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

(ii)Inapendekezwa kusamehe kodi ya *VAT* kwa chai iliyosindikwa (black tea) na iliyofungashwa *(Packaged Tea) i*li kuhimili ushindani baada ya soko la chai kufunguliwa. Lengo kubwa hapa ni kulinda pato la wakulima wadogo wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi katika Biashara Ndogo na za Kati. Eneo jingine litakalo patiwa msukumo maalum katika Bajeti hii ni la biashara ndogo na za kati *(SMEs)*. Baada ya sekta ya kilimo, inafuata sekta ya biashara ndogo na kati kuwa tegemeo kubwa la ajira kwa wananchi wengi. Aidha, sekta hii ni muhimu sana katika juhudi za Serikali za kuwawezesha wananchi kujiondolea umaskini. Kwa hiyo, mkazo mwingine wa Bajeti hii ni kuboresha mazingira kwa ajili ya kukua kwa sekta ya biashara ndogo na za kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa biashara ndogo na za kati zenye mauzo *(turnover)* isiyozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka hulipa aina mbili kubwa za kodi kwa *TRA,* ambazo ni Ushuru wa Stempu na Kodi ya Mapato kwa utaratibu wa kodi ya makadirio *(presumptive tax)*. Kodi hizo mbili zinakadiriwa kwa msingi wa thamani ya mauzo ya biashara husika. Ili kupunguza gharama kwa biashara hizi, inapendekezwa kufuta Ushuru wa Stempu na kufidia sehemu ya mapato yatakayopungua kwa kuongeza kidogo viwango vya kodi ya makadirio *(presumptive tax rates)*. Viwango vipya vya kodi ya makadirio vitakuwa kama ifuatavyo:

| **Thamani ya Mauzo (Shilingi)** | **Kodi iwapo kuna kumbukumbu za kuridhisha** | **Kodi iwapo hakuna kumbukumbu za kuridhisha** |
|---|---|---|
| 0 - 3,000,000 | 1.15% ya mauzo kwa mwaka | 35,000 kwa mwaka |
| 3,000,001 - 7,000,000 | Tshs. 35,000 na 1.3% ya mauzo | 95,000 kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| | yanayozidi Tshs. 3,000,000 kwa mwaka | |
| 7,000,001 - 14,000,000 | Tshs. 95,000 na 2.9% ya mauzo yanayozidi Tshs. 7,000,000 kwa mwaka | 291,000 kwa mwaka |
| 14,000,001 - 20,000,000 | Tshs.291,000 na 589,000 mauzo yanayomzidi Tshs. 14,000,000 kwa mwaka | 3.25% ya kwa mwaka |

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wasome orodha hii na kama ni wasilisho rasmi ni sehemu ya hotuba hii. Lakini inawezekana baada ya Majadiliano Serikali ikapokea mapendekezo kama yapo kwa orodha hii. Ningependa tu kukiri kupokea wazo hili kwa Mheshimiwa Mntangi tena kwa mara ya pili. Kwa sababu aliuliza swali hapa ingawa tulilijibu lakini jibu kamili liko hapa leo. Mwisho utaona kwamba kuna kodi iwapo hakuna kumbukumbu za kuridhisha. Kama kuna kumbukumbu kuna safu ya kodi. Kama hakuna kumbukumbu za kuridhisha kuna safu ya kodi. *(Makofi)*

Pamoja na kuwapunguzia mzigo wa kodi, utaratibu huu utatoa hamasa kwa wenye biashara hizi kutayarisha na kutunza kumbukumbu na hivyo kuongeza uwezekano wa kujenga mahusiano mazuri na wakopeshaji. Aidha, viwango vya kawaida vya Kodi ya Mapato kwa msingi wa faida halisi vitatumika pale ambapo hesabu kamili zitakuwa zimeandaliwa na kuwasilishwa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, vile vile inapendekezwa kuongeza kiwango cha chini *(threshhold)* cha mauzo kwa ajili ya usajili wa *VAT* kutoka shilingi milioni 20 hadi milioni 40 kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kuondoa biashara ndogo ndogo katika wigo wa *VAT* kwa kuzingatia gharama za kutunza mahesabu na pia gharama za kusimamia na kutawala ukusanyaji wa kodi hii. Hata hivyo, biashara zenye kiwango hiki cha mapato zitaweza kujisajili kama zikipenda yaani hawa wadogo wadogo wakipenda wajisajili lakini zitalazimika kufuata masharti ya Mamlaka ya Mapato *TRA* kuhusu uwajibikaji *(compliance)*. Hatua hii itaongeza tija ya *TRA* ya kusimamia ukusanyaji wa kodi hii kwa kuwa itaachana na utitiri wa walipa kodi wenye mchango mdogo kimapato. Hatua hii ikifanikiwa uamuzi kuhusu kiwango cha chini cha *VAT rate* hapo utakapofanikiwa utafanywa. Kushusha kiwango hicho kwa asilimia 2 tu kutailetea Serikali hasara ya shilingi bilioni 59 na kuathiri sana mapato ya kodi hiyo katika Bajeti. Ndiyo maana tumeona twende awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu linalolenga kuboresha mazingira na kuondoa kero kwa biashara, hasa ndogo na za kati linahusu ada za leseni za biashara chini ya Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972. Kwa kuwa nia ya leseni za biashara ni kusimamia tu kanuni za biashara kwa kutoa leseni *(regulatory)* na wala siyo chanzo cha mapato, hatua zifuatazo zinapendekezwa:

(i)Kufuta ada za leseni kwa hospitali, zahanati na vituo vya afya vinavyoendeshwa na asasi za dini ili kupanua huduma za afya zinazotolewa na asasi hizo. *(Makofi)*

(ii)Kufuta ada ya leseni inayotozwa chini ya Sheria ya Leseni za Biashara ya 1972 kwa biashara zenye mauzo yasiyozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka ili kupunguza gharama na kuwezesha vijana na wafanyabiashara wadogo kuanzisha biashara kwa njia halali. Biashara hizi zitapewa leseni bila kulipia ada. Biashara hizi zitapewa leseni bila kulipia ada. *(Makofi)*

(iii)Biashara zenye mauzo yanayozidi Shilingi milioni 20 kwa mwaka zitozwe ada ya leseni ya shilingi 20,000/= tu ili kupunguza gharama zinazoambatana na kuanza biashara, na kuweka mazingira mazuri ya kuingiza biashara nyingi katika Uchumi Rasmi. .Hii ni mambo ya Lesotho kama mtakumbuka. *(Makofi)*

(iv)Kufuta ada za leseni zinazotozwa chini ya Sheria ya Leseni za Biashara, pale ambapo biashara husika inasimamiwa chini ya Sheria nyingine ya kisekta ambapo leseni nyingine hutolewa chini ya sheria hizo. Mfano ni biashara ya kibenki, bima, n.k. Zitakazotumika ni leseni zinazoendana na sheria hizo na vyombo hivyo sio hii sheria ya 1972

(v)Leseni ya biashara chini ya Sheria ya Leseni za Biashara itolewe mara moja tu wakati biashara inapoanzishwa. Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, na Jiji zitakiwe kutayarisha na kutoa takwimu sahihi za leseni za biashara kwa mamlaka husika ili kuwa na takwimu pale zinapotakiwa kufanya hivyo. Kwa kweli Wizara ya Biashara inahitaji sana takwimu hizi na Wizara nyingine zinazoshughulika. Kwa hiyo, takwimu lazima ziwekwe na zipelekwe kunakohusika. Kwa kuwa wenye biashara wanasajiliwa pia na *TRA* kupitia Namba ya Utambulisho ya Kodi *(TIN),* hakuna haja ya kukata leseni ya biashara kila mwaka. *(Makofi)*

(vi) Pamoja na hatua hizi zinazohusu kodi na tozo nyingine mbalimbali, ningependa kueleza kwamba Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa ajili ya Biashara Ndogo na za Kati ulioanzishwa mwaka huu wa fedha umeongezewa fedha katika bajeti hii. Kanuni na taratibu za kutawala mfuko huo zimeshakamilika. Pamoja na hatua hizi za kuboresha sekta za kilimo na biashara ndogo na za kati, marekebisho mengine mapya katika kodi mbalimbali yanapendekezwa kama ifuatavyo:-

(i) Mfumo wa Kodi ya Mapato Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 iliyopitishwa katika kikao cha Bunge cha mwezi Aprili itaanza kutumika kuanzia Julai 2004. Inapendekezwa kwamba uandishi wa Sheria hiyo urekebishwe ili kufafanua kwamba Sheria hii itatumika kuanzia Julai 2004 kwa walipa kodi wote isipokuwa wale ambao wanatengeneza mahesabu na ambao mwaka wao wa mapato ulianza kabla ya Julai 2004.

(ii) Mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*

(a) Ili kuwezesha wazalishaji wa ndani kurejeshewa *VAT* wanayolipa kwa malighafi, inapendekezwa kujumuisha madawa ya binadamu na mifugo, vyandarua, na vifaa maalum vya walemavu katika Jedwali la I ili zisilipiwe kodi kwa kuwa kwenye kiwango cha sifuri *(Zero Rate).* .yaani hizi kwenye vitabu vya forodha vitawekwa kwenye viwango vya sifuri na kwa hiyo havitalipiwa kodi. *(Makofi)*

(b) Kurekebisha msamaha wa kodi kwa magari kwa wale wenye msamaha huo, ili kujumuisha magari yaliyomo kwenye *HS Code* 8703, 8702.10.20 na 8702.90.20 yenye injini zenye uwezo zaidi ya *CC 3000*. *(Makofi)*

Pamoja na hatua nilizoeleza awali, marekebisho haya katika mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* yatapunguza mapato ya Serikali kwa shilingi 4,954 milioni.

Hatua mpya nilizozitaja zina lengo la kuimarisha kilimo na biashara na kuwezesha wananchi, hasa wale wa kipato kidogo kuingia katika uchumi rasmi na kujitafutia riziki ili wajiondolee umaskini. Aidha, marekebisho katika ada za leseni yanajibu pia hoja za wawekezaji na Wafadhili wetu ambao ni pamoja na taasisi za dini zinazotoa huduma ya jamii Nchini mwetu.

(iii) Mfumo wa Ushuru wa Bidhaa

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho kadhaa katika eneo la ushuru wa bidhaa kama ifuatavyo:

Kwanza. kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kulingana na mfumuko wa bei kwa bidhaa zifuatazo:

(1) Vinywaji baridi. Ushuru unaongezwa kutoka shilingi 37.50 kwa lita hadi shilingi 40.0 kwa lita. *(Makofi)*

(2) Bia. Ushuru unaongezwa kutoka shilingi 232.0 kwa lita hadi shilingi 243.0 kwa lita. *(Makofi)*

(3) Mvinyo. Unaotengenezwa kwa kiwango kisichozidi asilimia 75 ya zabibu inayozalishwa hapa nchini. Ushuru unaongezwa kutoka shilingi 743.40 kwa lita hadi shilingi 780.00 kwa lita. *(Makofi)*

(4): Vinywaji vikali. Ushuru unapanda kutoka shilingi 1,102.50 kwa lita hadi shilingi 1,158 kwa lita. *(Makofi)*

(5) Sigara zenye urefu usiozidi milimita 70 na zinazotengenezwa kwa tumbaku inayozalishwa nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75. Ushuru unaongezwa kutoka shilingi 3,781.05 kwa sigara 1000, hadi shilingi 3,970 kwa sigara 1000.

(6) Kwa sigara zenye urefu wa milimita 70 au zaidi zilizotengenezwa kwa kiwango cha tumbaku inayozalishwa nchini inayozidi asilimia 75. Ushuru unaongezwa kutoka shilingi 8,920.30 kwa sigara 1000 hadi shilingi 9,367 kwa sigara 1000. *(Makofi)*

(7) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na nilizozitaja katika vifungu vya (tano) na (sita) hapo juu, ushuru utaongezeka kutoka shilingi 16,206.75 kwa sigara 1000 hadi shilingi 17,017 kwa sigara 1000. *(Makofi)*

(8) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *"cut rug/filler"* ushuru wake unaongezeka kutoka shilingi 8,183.70 kwa kilo hadi shilingi 8,593.

(9) Ushuru wa "Cigar" unabaki kuwa asilimia thelathini (30%). *(Makofi)*

Pili, kuweka ushuru wa bidhaa (excise) kwenye huduma ya televisheni kupitia satelaiti *(DSTV)* kwa kiwango cha asilimia 5 kwa mauzo ya huduma hiyo. Yaani hizi ni zile *TV* za kulipia, sio hizi ndogo ndogo.

Mwisho, kurekebisha msamaha wa ushuru wa bidhaa kwa magari ili kuingiza magari yaliyomo kwenye *HS Code* 8703, 8702.10.20, na 8702.90.20 yenye injini zenye uwezo zaidi ya *CC 3000.*

Marekebisho haya ya Ushuru wa Bidhaa yataiongezea Serikali mapato ya shilingi milioni 6,143.

Nne, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa:

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuzipa uwezo Halmashauri kukusanya mrahaba *(royalty)* kwenye madini ya Jasi *(Gypsum),* Pozzolana, na Chokaa, ambayo yanatumiwa na viwanda kama malighafi. *(Makofi)*

Tano. Ada ya Leseni za Biashara zinazokusanywa na Wizara na Vyombo Vingine vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua nilizoainisha awali katika eneo hili kwa pamoja zitaipunguzia Serikali mapato kwa kiasi cha shilingi milioni 14,000, ambazo zimegawanyika kama ifuatavyo:-

Shilingi milioni 11,200 kwa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, na shilingi milioni 2,800 kwa Wizara ya Viwanda na Biashara. Bajeti hii imetenga fedha hizo kufidia Halmashauri na Wizara hiyo.

Sita Ada ya Viza na Utaratibu wa kutoa Viza:

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wageni wanaoingia Tanzania kama wafanya-biashara wanalipa ada ya viza ya dola za Marekani 200 na wale wanaoingia kama Watalii au wasafiri wa kawaida wanalipa ada ya viza ya dola za Marekani 50.

Kwa kuwa dola 200 ni nyingi na kwa kuzingatia tofauti kubwa kati ya dola 200 na 50, wageni wengi waingiapo nchini wanajitambulisha kama wasafiri au watalii wa kawaida. Hivyo ni wachache sana wanaolipa ada hiyo ya dola za Marekani 200.

Aidha, kuna ufujaji mkubwa wa mapato yatokanayo na ada ya viza unaosababishwa na utaratibu unaotumika wa kutoa viza kwa wageni wanaokuja nchini kwetu.

Utaratibu unaotumika ni wa kupiga muhuri kwenye pasi ya kusafiria, ambao imedhihirika hauna udhibiti na ni wa kizamani. Kwa sababu hizi, inapendekezwa kama ifuatavyo:-

(i) Ada ya viza ya biashara ya Dola za Marekani 200 ipunguzwe hadi Dola za Marekani 50 ili kuondoa tofauti hiyo ambayo haina faida kwa nchi yetu ambayo inataka itembelewe na wawekezaji wengi, wafanyabiashara wengi na watalii kemkem. *(Makofi)*

(ii) Utaratibu mpya wa kutumia visa stickers uanzishwe badala ya huu wa sasa wa mihuri, ili kudhibiti mapato yatokanayo na viza nchini na katika Balozi zetu. Hatua hizi mbili kwa pamoja zitaipatia Serikali mapato mapya ya Shilingi milioni 19,823. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfumo wa Ushuru wa Forodha, yapo marekebisho matatu katika eneo hili. Mfumo wa Ushuru wa Forodha utabadilika kutokana na makubaliano yaliyofikiwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha *(East African Customs Union)*. Mabadiliko hayo ni pamoja na: -

(a) Kuondoa ushuru wa forodha kati ya nchi wanachama kwa awamu kwa utaratibu uliokubalika na pia kuwa na viwango sawa vya ushuru kwa bidhaa kutoka nje ya Afrika Mashariki. Aidha kanuni na taratibu za forodha zitawianishwa ingawa kila nchi mwanachama wa Jumuiya itaendelea kusimamia forodha yake na kukusanya ushuru wake. Mkataba wa Umoja wa Forodha utaanza kutekelezwa baada ya kuridhiwa na Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya. Inategemewa kwamba umoja huo wa forodha utaanza kutumika Januari 1 mwakani na hatua hii itatupatia mapato ya ziada ya Shilingi milioni 5,949 mwaka huu wa fedha wa 2004/2005.

(b) Kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ushuru wa muda *(Suspended Duty)* unaotozwa kwa bidhaa kutoka nje ya nchi utafutwa isipokuwa zile bidhaa ambazo zimekubaliwa ziendelee kutozwa ushuru huo ndani ya mkataba. Hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha Shilingi milioni 4,811 mwaka 2004/2005.

(c) Msamaha wa ushuru wa forodha kwa magari unarekebishwa ili kuingiza magari yaliyomo kwenye *HS Code* 8703, 8702.10.20 na 8702.90.20 yenye injini zenye uwezo zaidi ya *CC 3,000* kwa pamoja. Hatua zote katika ushuru wa forodha zitaiongezea Serikali mapato kwa Shilingi milioni 1,138 katika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya sheria nyingine za kodi, inapendekezwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za kodi ili ziendane na wakati na kurahisisha utekelezaji wake, sheria hizo ni zifuatazo: Sheria ya kodi ya mapato, sheria ya kodi ya ongezeko la thamani, sheria ya ushuru wa forodha, sheria ya ushuru wa bidhaa , sheria ya ushuru wa stempu, sheria ya leseni za biashara, sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa, sheria ya mafunzo ya ufundi stadi na sheria ya biashara ya michezo ya kubahatisha. Marekebisho hayo hayatarajiwi kuwa na athari kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda kodi mpya kutumika ni kwamba hatua hizi za kodi mpya zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2004 isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho yote yanayopendekezwa ni kuboresha mazingira ya kukuza uchumi wetu, kuwawezesha Wananchi kufanya shughuli mbalimbali za kujiendeleza na kujiondolea umaskini na kupanua wigo wa ajira na kodi. Aidha, baadhi ya hatua hizi zitaongeza na nyingine zitapunguza mapato ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha, kama ifuatavyo: -

(i) Mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani utapunguza mapato kwa Shilingi milioni 4,954.

(ii) Mfumo wa ushuru wa bidhaa utaongeza Shilingi milioni 6,143.

(iii)Mfuko wa kodi ya mapato utaongeza mapato kwa Shilingi milioni 13,189.

(iv)Mfumo wa ushuru wa forodha utaongeza mapato kwa Shilingi milioni 1,138.

(v)Mfumo wa ushuru wa stempu utaleta hasara kwa Serikali ya Shilingi milioni 19,263.

(vi)Mfumo wa tozo la ufundi stadi utailetea Serikali hasara ya Shilingi milioni 2,076 .

(vii) Mfumo wa leseni za biashara utaleta hasara kwa Shilingi milioni 14,000;na

(viii)Mfumo wa viza utaleta faida kwa Shilingi milioni 19,823.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti nilioueleza hapo juu sura ya bajeti ya mwaka 2004/2005 inakuwa kama ifuatavyo: -

Mapato ya ndani ni Sh.1,739,288,000,000/= kutokana na mapato ya kodi 1,603,886 milioni, mapato yasiyo ya kodi 135,402 milioni na pia mapato yatatokana na mikopo na misaada ya nje ikijumuisha misaada ya misamaha ya madeni ambayo ni Sh.1,367,025,000,000/=. Pia, mapato kutokana na uuzaji wa hisa Sh.10,115,000,000/= na kupunguza akiba *(reserve)* pamoja na mikopo ya ndani Sh.231,110,000,000/= na jumla ya mapato yote ni Sh. 3,347,538,000,000/= .

Matumizi yatakuwa kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida ni Sh.2,239,000,000,000/=. Haya yatakuwa ni kwa ajili ya deni la Taifa, Wizara (Sekta mbali mbali), Mikoa, Serikali za Mitaa, matumizi maalum yaani mishahara kwenye Taasisi, mishahara kwenye Serikali Kuu, *Tansort Escrow Account,* vita dhidi ya rushwa na mafao ya watumishi. Matumizi ya Maendeleo ni Sh.1,091,590,000,000/= ambazo ni fedha za ndani na fedha za nje na dharura Sh.16,948,000,000/= na hiyo inatumia fedha zote tulizozipata kule mwanzoni kwenye mapato.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyosema awali, bajeti ya mwaka 2004/2005 imeandaliwa kwa msingi wa kuendeleza juhudi za Serikali katika kutekeleza:-

(i) Shabaha za Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000 ya Chama Cha Mapinduzi. *( Makofi)*

(ii) Dira ya Taifa ya Maendeleo hadi 2025. *(Makofi)*

(iii) Mkakati wa Kupunguza Umaskini. *(Makofi)*

(iv) Sera za Kijumla za Kiuchumi kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Sekta ya Kilimo ina uwezo mkubwa wa kutoa ajira kwa Wananchi wengi iwapo yatafanyika mapinduzi zaidi katika Sekta hii. Serikali imejitahidi kufanya yale yanayowezekana kwa uwezo uliopo. Sasa ni juu ya Wananchi, pamoja na wawekezaji wa ndani na wa nje kutumia fursa hii ili kuinua Sekta hii. Aidha, Sekta ya Viwanda pia ina uwezo wa kuongeza Pato la Taifa na ajira kwa haraka kama itapewa msukumo wa kutosha. Ili kupata mafanikio ya wazi, msukumo katika ukuzaji wa uchumi lazima uwe wa dhati kabisa. Bajeti hii inalenga kuweka misingi mizuri kwa Sekta ya biashara ndogo ndogo na za kati ili iweze kuibuka na kujaza pengo dhahiri katika uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika yote haya, mafanikio halisi ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini yatapatikana pindi tutakapoweza kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati. Pili, tunahitaji kujenga uwezo wa utaalam ambao ni lazima katika dunia hii ya utandawazi. Tatu, kwa kuwa Wananchi wengi wanaishi vijijini na wanategemea kilimo kwa chakula na ajira, ni lazima mkakati wetu wa kuinua kilimo uwe imara zaidi na uunganishe kilimo, viwanda na biashara, ndipo tutaweza kugeuza Sekta hiyo iwe ya kisasa *(Modernization of Agriculture).* Pengine tuna haja ya kuangalia tena vipaumbele vyetu ili tupate tija ya uhakika kwa kutumia uwezo mdogo tulionao wa fedha kwa maeneo machache kwanza kuliko kugawa

kidogo kidogo bila mafanikio ya maana, yaani bila impact. Nitafurahi kupata ushauri wa Waheshimiwa Wabunge juu ya wazo hili wakati wa mjadala wa hoja hii. Kugawa kidogo kidogo, ama kugawa kwa wingi kwa mpigo kupata impact kwa muda mfupi. Hii ndiyo hoja kubwa katika matumizi ya bajeti hii na nyingine zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni mfululizo wa jitihada za Serikali ya Awamu ya Tatu za kurekebisha uchumi na kupambana na umaskini. Inaendeleza matakwa ya uchumi tulivu, endelevu na unaokua hatua kwa hatua, mwaka hadi mwaka. Inaweka mazingira mazuri ya kujiajiri, kuwekeza na kujiendeleza. Inatoa fursa kwa kila mtu kufanya kazi kwa tija, hasa za kilimo na shughuli ndogo ndogo. Inawezesha Wananchi waliokwishaanza safari ya kujiajiri na kujitegemea kiuchumi kupiga hatua zaidi, kwa kuwaondolea urasimu, kuwadhamini wakikopa benki, kuwapunguzia kodi, leseni na ushuru wa aina aina na kuwaondolea kero ya kufukuzana na wakata leseni, hasa wa mijini. Naamini kuwa hotuba zifuatazo za Mawaziri wa Kisekta zitatangaza hatua zaidi za kuwawezesha Watanzania kujiendeleza kiuchumi na kijamii katika Sekta zao kwa mujibu wa sera iliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo hakuna Serikali inayoweza kumlisha au kumtajirisha mwanakaya ambaye hachukii umaskini na kufanya kazi kwa bidii. Hakuna Serikali ya namna hiyo! Uchumi wa kaya na wa Taifa unakuzwa na wanakaya na Wananchi kwa ujumla wao. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kumwezesha mwenye nia na dhamira ya kupiga hatua ya maendeleo ya kaya yake na ya Taifa lake. Naamini kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaelewa sana ninachosema na hivyo natumaini watakuwa radhi kuniunga mkono kwa kura zao za moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Waziri wa Fedha imetolewa na imeungwa mkono na kwa taratibu zetu za kawaida, hoja zote mbili zilizotolewa leo zitajadiliwa kuanzia siku ya Jumatatu. Kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa na Kamati yetu ya Uongozi siku ya kesho haina kikao na hii ni kwa madhumuni ya kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wazitafakari hotuba hizi za leo, wazisome, wazipitie vizuri na kujiandaa kwa michango yao itakayoanza Jumatatu.

Kwa kuwa kesho hakuna kikao, bora nitoe tangazo ambalo lingetolewa kesho nalo linahusu semina ya kesho kutwa siku ya Jumamosi. Tumeandaa semina inayodhaminiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, inahusu Mkakati wa Kupunguza Umaskini, itaanza saa tatu asubuhi kama kawaida kwa masharti yale yale ya kawaida. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni za Bunge, sasa naahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.43 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 14 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*